## Kinachompata mke aliye na dharau kwa wakwe, ndugu

UKURASA 11



## Adaiwa kujiua kwa kujikata shingo akitumia mashine ya mbao

UKURASA 8




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 18, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • No. 0581345

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Kumekucha vigogo mashirika ya umma

• **Rais** Samia atangaza kuwafuta kazi wasiozalisha faida... *Uk. 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akipokea gawio la serikali la zaidi ya Sh. bilioni 45.5 kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede (wa pili kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna (wa pili kushoto) wakati wa hafla ya kuadhimisha miaka 25 ya mafanikio ya benki hiyo mkoani Dar es Salaam jana. Katikati ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na kushoto ni Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA
### GARI LINALOHUSISHWA LAPELEKWA MAHAKAMANI

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imepokea kielelezo cha gari aina ya Landrover lenye namba za usajili...

UKURASA WA 4

### AHUKUMIWA KUNYONGWA KWA KUMUUA MNYWAJI MWENZAKE

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Tabora imemhukumu Mwande Punguja (36), mkazi wa Kijiji cha Mwitungu, Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora...



## Zitto aibua maeneo manane yenye dosari bajeti ya 2023/24

UKURASA 3

## Polisi yawaonya waliopanga kuandamana sakata la Bandari

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA SC YAANZA MAKEKE UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6


Kamanda Jumanne Muliro.

# Polisi waonya maandamano sakata uendeshaji Bandari

**Na Beatrice Shayo**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limepiga marufuku maandamano yaliyopangwa kufanyika kesho jijini kuelekea Ikulu ya Magogoni.

Kauli ya jeshi hilo imekuja baada ya kuwapo mtu anayehamasisha katika mitandao ya kijamii maandamano hayo siku ya kesho ili kupinga makubaliano ya uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam yaliyoingiwa kati ya Tanzania na Dubai kupitia Kampuni ya DP World.

Mhamasishaji huyo pia anataja sababu nyingine ya kuandamana ni kupinga muswada wa sheria ya masuala ya usalama kuwekewa kinga ya baadhi ya watendaji kushtakiwa kwa makosa ya jinai.

Kutokana na kuwapo kwa hamasa hiyo, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, jana alikiri kuwa na taarifa hizo za kuitishwa maandamano Juni 19 mwaka huu (kesho).

Alisema taarifa hiyo imeshawafikia na tayari wamempatia majibu mtu huyo na kumshauri kuwa kama ana jambo la msingi, atumie vyombo mbalimbali vya kisheria kuwasilisha hoja zake bila maandamano ili haki zingine za wananchi za kufanya kazi wakiwa huru zisiingiliwe.

"Jeshi la Polisi linawatahadharisha watu kutoshiriki hicho kinachodaiwa maandamano na badala yake, wanahimizwa kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii bila hofu," alisema Kamanda Muliro.

Alisema Jeshi la Polisi halitosita kuchukua hatua kwa mtu au kundi linalotaka kuzusha taharuki kwa kuzuia watu wengine kufanya kazi zao.

Kamanda Muliro pia alisema wanawashikilia watu 10 wanaodaiwa kuhujumu miundombinu kwa kuiba vifaa mbalimbali vya minara ya mawasiliano ya simu.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa kupitia operesheni iliyoanza Juni 5 mwaka huu na inaendelea katika jiji hilo la kibiashara, ikihusisha pia mikoa jirani.

# Kumekucha vigogo mashirika ya umma

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema amepokea ripoti ya awali kuhusu hali ya mashirika ya umma, akimpa kazi ya mwisho Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, kumalizia tathmini ili achukue uamuzi mgumu.

Alitangaza hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akifunga maadhimisho ya miaka 25 ya Benki ya NMB na kukabidhi serikalini gawio la Sh. bilioni 45.5 kutokana na faida waliyoitengeneza mwaka 2022 ya zaidi ya Sh. bilioni 429.

"Kama alivyosema Msajili wa Hazina, serikali tumeamua kufanya tathmini ya utendaji wa mashirika yote ya umma na yale ambayo serikali ina hisa kubwa. Lengo ni kubaini mashirika yasiyo na faida ambayo yameshindwa kujiendesha na yanaitia serikali hasara," alifafanua.

Rais Samia alisema Msajili wa Hazina amefanya tathmini ya awali na kumpelekea ripoti na amemwagiza aende kufanya tathmini ya pili.

"Kwa hiyo, wale mnaoshika mashirika, hapa TFS (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania) ninakuona (Prof) Dos Santos (Silayo - Mtendaji Mkuu wa TFS), kajitazame vizuri ndani ya shirika lako pamoja na kwamba misitu ni wewe peke yako, hebu kajitizame vizuri.

"Na wale wote mnaoshika mashirika, nendeni kajitazameni vizuri. Hii haina kurudi nyuma, kuna ambayo tutayafuta, kuna ambayo tutayasaidia, kuna ambayo tutayapa miongozo namna ya kujiendesha ili wote mfanye kwa faida.

"Serikali imeunda mashirika haya ili yasaidie kutengeneza fedha zitakazosaidia kubeba mzigo wa serikali na si mashirika ya kula serikalini bila kurudisha faida ambayo mengi yapo ya aina hiyo.

"Kwa hiyo, Msajili (wa Hazina) vaa njuga, nimekupa baraka zote. Ninasubiri taarifa za mwisho ya mashirika gani yanabaki na yapi yanaondoka na yapi yasaidiwe vipi kufanya biashara.

"Na siku tutakapoyatangaza, yale ambao tutatoa fedha mfukoni kuyapa na kuyasaidia, nitawaambia kama nilivyomwambia Mhede kwamba, haya mashirika yakifa wafe nayo.

"Sitaki kusikia shirika linazorota, meneja anapiga suti nzuri anatamba mitaani," Rais Samia alionya.

**WAJASIRIAMALI**

Kwa wajasiriamali wanaopata mikopo, Rais Samia aliwakumbusha kwamba wameaminiwa na wajiaminishe wanapoichukua wakumbuke kurudisha bila kusimamiwa kama walivyochukua awali.

"Hii ni benki, imefanya vizuri sana, tusiende kuiua, tusiende kuiangusha. Msajili wa Hazina endelea kuyasimamia mashirika yetu, tunataka mashirika yote ya umma na yale ambayo serikali ina hisa kubwa yanajiendesha kwa ufanisi," aliagiza.

Kuhusu NMB, Rais Samia alionyesha kufurahishwa na utendaji kazi wake chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna na Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Edwin Mhede, huku akiwaeleza kuwa wanastahili kusherehekea miaka 25.

Mkuu wa Nchi aliipongeza benki hiyo kwa hatua kubwa iliyopiga, hata kufikia kutoa gawio kubwa serikalini.

"Niwapongeze katika gawio mlilojipanga mwaka huu. Na kati ya hizo Sh. bilioni 2.5 zimepangwa kwa ajili ya shule maalum kwa mkoa nitakaochagua, nitazitolea maelekezo, asanteni. Mnastahili pongezi kubwa na mna haki ya kusherehekea miaka 25.

"Iliposimamishwa bodi niliona kuna wanawake watatu, hebu wasimame. Hakuna wanawake kwenye bodi, menejimenti hapa ndo niliona wanawake angalau wawili watatu na ukiongeza na Mtendaji Mkuu mambo yanakwenda.

"Kuna utafiti unasema taasisi inayokuwa na menejimenti inayoanza na wanawake watatu hiyo taasisi inafanya vizuri, ni utafiti uliofanywa Tanzania kuhusu mashirika ya umma.

"Kwa hiyo, hii bodi inafanya vizuri kwa kuwa menejimenti ina wanawake, mtendaji mkuu mwanamke, ni ujumbe wangu bodi ijayo wanawake wawamo," aliagiza.

Rais Samia pia alimpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya NMB kwa kudhihirisha umahiri ndani ya benki hiyo, akisema alikutana naye juzi na wakazungumza kuhusu Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART). Anaona mageuzi aliyofanya na malengo ya baadaye.

"Juzi nilimwambia hili shirika likifa ufe nalo, na leo ujumbe ni huohuo. Hii benki ikifa ufe nayo," Rais Samia alionya.

Alisema NMB ni benki kiongozi katika kutengeneza faida na imeiweka nchi katika ramani kwa kuwa ya tatu kwa faida katika sekta ya kibenki ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ya kwanza kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na hati fungani maalum inayomlenga mwanamke.

"Ninawashukuru kwa kuja na wazo hili, linaibeba safari yangu ya uchampioni kwenye suala la generation equality (usawa katika jamii), nimekuwa balozi wa hili kwa ulimwengu toka nimeingia kuwa Rais, mfano wangu ni nchi yangu namna tunavyokwenda na usawa wa kijinsia. Hii inakwenda kunibeba vizuri ninapokuwa kwenye mikutano," alisema.

Rais Samia pia alisema amearifiwa kupitia hati fungani, benki imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 74 zilizoelekezwa katika biashara zinazoongozwa na wanawake.

Alisema NMB pia wametenga zaidi ya Sh. bilioni 200 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo na mnyororo wa thamani kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Alisema gawio la Sh. bilioni 45.5 linatokana na hisa za serikali kupitia mambo makubwa yaliyofanywa na NMB mwaka 2022, faida ikiwa ni zaidi ya bilioni 429.

Mkuu wa Nchi alikumbusha kuwa mwaka jana, serikali ilipokea gawio la Sh. bilioni 30.6 na sasa limekua hadi kufikia Sh. bilioni 45.5.

Alisema mchango wa kodi kwa serikali ulikuwa Sh. bilioni 383 ndani yake ikiwamo kodi ya ujuzi, VAT na kodi ya mapato na nyinginezo.

Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Zaipuna, alisema hafla hiyo ni kielelezo bora cha mambo makubwa matatu, ambayo ni matunda ya ubinafsishaji na mabadiliko chanja ya misingi wezeshi ya kiuchumi, kibiashara na kijamii na kuchagiza ukuaji wa uchumi ikiwamo benki hiyo.

Pia alisema ni uwekezaji wa kimkakati uliolenga kuijenga NMB shindani na endelevu yenye misingi imara ya utawala bora, kiutendaji na kiufanisi.

"Mheshimiwa Rais, jambo la tatu hafla hii ni kielelezo cha imani kubwa ya wadau wa NMB, iliyowezesha kuijenga benki imara kwa maendeleo ya watu, benki yenye tija kwa wateja wake, wawekezaji na jamii kwa ujumla," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kwa sasa wana matawi 227 kulinganishwa na matawi 97 mwaka 1997 wakati benki ilipoanzishwa, mashine za ATM 7,081 na mawakala 23,679 na akaunti za wateja milioni 6.3 kulinganishwa na akaunti chini ya 600,000 walizokuwa nazo awali.

Alisema uwekezaji mkubwa wa teknolojia uliofanyika, umefanya kwa sasa miamala ya kibenki kwa asilimia 94 kufanyika nje ya benki.

Alisema mwaka 2022, benki ilipata tuzo 23 za kitaifa na kimataifa, zikiifanya NMB itambulike kuwa ni taasisi bora.

"Mwaka 2009 tulitoa gawio la Sh. bilioni 4.9, sasa hivi tunakwenda kutoa Sh. bilioni 45.5 kwa mwaka 2022, hili ongezeko ni sawa na asilimia 911 katika kipindi hiki cha marejeo kutoka 2009-2022.

"Hii inafanya kuwa gawio kubwa zaidi kuwahi kutolewa na taasisi yoyote ya kifedha kwa serikali," alitamba.

Alisema mwanahisa anayemiliki asilimia 34.9 ameshalipwa Sh. bilioni 49.9 na wanahisa wote wanaomiliki asilimia 33.3 wamelipwa Sh. bilioni 47.7, na kufanya jumla la gawio lote walilolipa kwa wanahisa kwa mwaka huo kuwa Sh. bilioni 143.1 kutoka Sh. bilioni 96.7 mwaka jana.

Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Mhede, alisema aina ya ubinafsishaji uliofanyika imefanya benki kujenga mizizi imara kwa wateja.

Msajili wa Mhazini, Mchechu, alisema maagizo ya Rais kwao ya kuangalia taasisi za kuzifuta, kuziunganisha, kuziboresha litakwenda kufanyika kwa kuangalia maslahi ya nchi na si kutazama sura.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema katika bajeti ya 2023/24, serikali imeweka Sh. trilioni moja inayokwenda kukuza sekta binafsi. Aliutaja ni uamuzi wenye maana kubwa, hata wenye mikopo chechefu watakwenda kuilipa.

Alisema gawio lililotolewa litatumika katika utekelezaji wa bajeti ya serikali.

HABARI KITAIFA

BAJETI 2023/24

# Zitto: Nzuri kwa wafanyabiashara, shida kwa wananchi wa hali ya chini

Na Halfani Chusi

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha yaliyowasilishwa bungeni Alhamisi yanalenga kutoa unafuu kwa wafanyabiashara, lakini yamewatelekeza wanyonge.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwasilisha bungeni jijini Dodoma mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Katika uchambuzi wake, Zitto amesema anaona mapendekezo hayo hayalengi kutoa unafuu kwa wanyonge.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam baada ya kuchambua mapendekezo hayo, Zitto alitaja maeneo manane yenye dosari akisisitiza yatawafanya wananchi wa hali ya chini wateseke zaidi.

Maeneo hayo ni kutokufikiwa kwa malengo ya makusanyo ya kodi kwa mwaka 2022/23 na kuhoji fedha za bajeti kwa mwaka 2023/24 zitakakotoka.

Aliitaja ni bajeti isiyojibu changamoto za wananchi.

Zitto aliyataja maeneo mengine ni uhaba wa fedha za kigeni, mikopo ya kibiashara inayoligharimu taifa, marekebisho ya kodi, tozo na makato ambayo alisema ni furaha kwa 'vibonge' na vilio kwa wanyonge.

Pia alisema kodi kwa wafanyakazi na waajiri bado ni mzigo, pia akimulika mgawanyo wa fedha za Muungano.

Zitto alisema mapendekezo ya bajeti hiyo hayajajibu changamoto za wananchi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, ukosefu wa ajira kwa vijana, upatikanaji duni wa huduma za afya, elimu na maji.

"Ili kujibu changamoto hizi, hatuna budi kutazama sera za kibajeti katika kuchukua hatua za kukabiliana na kupanda kwa gharama za maisha kwa kutazama maeneo yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira nyingi na kuona kama uamuzi wa kibajeti unapeleka rasilimali kwenye maeneo ya kilimo na viwanda," alisema.

Zitto alisema asilimia kubwa ya wananchi wanakufa kwa kile alichokiita umaskini na wengine kwa magonjwa yanayoweza kutibika.

"Huduma mbovu za afya ni chanzo kikubwa cha umaskini kwa watanzania. Kwa mujibu wa utafiti wa Benki ya Dunia (WB), watanzania wengi wapo juu kidogo au chini kidogo ya mstari wa umaskini.

"Wakipata changamoto za afya walio juu ya mstari wa umaskini hurudi chini na walio chini huenda chini zaidi. Bima ya afya ni nyenzo muhimu sana kuzuia watu kudumbukia kwenye umaskini," alisema.

Zitto alisema kwamba mfumo wa bima ya afya wa sasa ni wa kitabaka ambao unatoa huduma kulingana na uwezo wa mtu badala ya kuangalia mahitaji yake.

Alisema mapendekezo ya bajeti kwa mwaka ujao wa fedha, hayajalitazama tatizo hilo ili kutenga fedha za kuweka mfumo mzuri na endelevu wa kufadhili wa bima kwa watanzania wote na kuwezesha kugharamia matibabu.

Waziri Kivuli wa Fedha na Uchumi wa chama hicho, Ester Thomas, alizitaja njia ambazo serikali inapaswa kuzitumia kumaliza dosari hizo kuwa ni kufuata katiba ya nchi kwa kuanzisha akaunti ya pamoja ya fedha kwa mujibu wa sheria na mapato yote ya Muungano yawekwe humo.

Pia alipendekeza kufanya utafiti mpya wa mapato ya Muungano na matumizi ya shughuli za Muungano ili kupata takwimu za sasa. Serikali igawe ziada za mapato ya Muungano kwa washirika wa Muungano.

"CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali) afanya ukaguzi maalum wa fedha za Muungano, mapato, matumizi na fedha zinazobakia, ili kubainisha mgawo sahihi ambao Zanzibar inastahiki," alisema.

Alitaja mapendekezo mengine ni tozo za miamala ya simu ziwe kama ilivyokuwa kabla ya mwezi Julai mwaka 2021, ili kuwapunguzia mzigo wananchi na kuondoa kabisa kodi ya asilimia mbili wachimbaji wadogo.

Pia alipendekeza kubadili Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ili kurejea makato ya asilimia nane ya kulipa mkopo huo kama ilivyokuwa kabla ya mwaka 2016 badala ya asilimia 15 ya sasa.

"Magari yote ya serikali yaanze kutumia gesi asilia, ili kupunguza kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa za mafuta. Pendekezo hili litapelekea kupunguza matumizi ya serikali kwa takribani Sh. bilioni 500 kwa mwaka," alisema.

Alisema ACT-Wazalendo pia inapendekeza kuharakishwa kwa mradi wa gesi asilia Mkoa wa Lindi na kuufungamanisha na mradi wa kuanzisha kiwanda kikubwa cha kuzalisha mbolea ili wakulima na wafanyabiashara wanufaike zaidi.




Kiongozi wa Chama Cha ACT-WAZALENDO, Zitto Kabwe, akizungumza wakati wa mkutano wa kuchambua Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024, iliyotolewa Bungeni na Waziri wa Fedha hivi karibuni, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**


**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**

**(CAP. 117)**

**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL.**

BY THIS DEED, I **BONIFACE WILSON MBULI** OF P. O. Box 50 KIDATU DO HEREBY wholly, absolutely and utterly renounce, relinguish and abandon the the use of the former name of BONIFACE P. WILSON and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of the former name, the name of **BONIFACE WILSON MBULI** for the purpose of evidanceof such determination, I, hereby DECLARE that hi will at all times hereinafter in all records, deed, documents and otherwriting and in all action, suits and proceedings as well as in all Publis and Private dealings and transactions and creations whatsover use and subscribe the said name of **BONIFACE WILSON MBULI** appear on my National Identification Card with No. 19671125-67508-0000-426 in lieu of and in submition for the former names of **BONIFACE P. WILSON**
AND I HEREBY expressly authorize and require all and every person and whatsover at all times after the date hereof to designeted describe and adress him by the adopted name of **BONIFACE WILSON MBULI**
IN WITNESS WHERE of I have set my hand at MOROGORO, and I hereon substitute the old name of **BONIFACE P. WILSON** by the new name **BONIFACE WILSON MBULI**

SIGNED and DELIVERED by the said BONIFACE WILSON MBULI who is known to me personally/identified to me by ............ the latter being known to me personally in my presence this 26th day of May 2023

DEPONENT



BEFORE ME:
Signature: ..........
Postal Address: ..........
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**
**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

# Ahukumiwa kunyongwa kwa kumuua mnywaji mwenzake

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Tabora imemhukumu Mwande Punguja (36), mkazi wa Kijiji cha Mwitungu, Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua Kagwa Alusha (35) kwa kumtumbukiza kisimani baada ya kutoka baa kunywa pombe.

Akisoma hukumu hiyo juzi, Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Tabora, Jovith Kato, aliyekasimishwa mamlaka ya jaji, alisema mshitakiwa alitenda kosa hilo Februari 6 mwaka huu katika Kijiji cha Mwitungu wilayani humo.

Alieleza kuwa wawili hao waliokuwa wakinywa pombe katika moja ya baa, waliondoka pamoja huku Alusha akiwa amebebwa kwenye baiskeli na Punguja.

Hakimu huyo alisema kuwa baada ya kufika eneo la kisima kirefu, Punguja aliamua kumdumbukiza kisimani na kumsababishia umauti kisha yeye kuendelea na shughuli zake bila kujali ukatili aliomtendea mwenzake.

Hakimu Kato alieleza kuwa kutokana na kosa hilo, mahakama hiyo ilimtia hatiani na kumhukumu kunyongwa hadi kufa kutokana na ukatili na kuondoa uhai wa mwenzake kwa makusudi.

Awali mshtakiwa alipohojiwa kuhusu mashtaka hayo, alikubali na kukiri kutenda kosa hilo la kumtumbukiza kisimani na kumsababishia kifo chake bila kujali kuwa mtu huyo alikuwa na familia inayomtegemea.

Akitoa ushahidi wake kuhusu tukio hilo, mmoja wa mashahidi wa upande wa Jamhuri, Kundi Ngelela ambaye walikuwa naye kwenye baa, alidai Alusha alibembwa na mshitakiwa kwenye baiskeli yake na kuondoka naye.

Shahidi huyo alisema kwamba alipofika nyumbani kwake, alitoka kwenda kwa Alusha hakumkuta ndipo alipoingiwa na wasiwasi. Wakaanza kumtafuta na wanafamilia sehemu mbalimbali bila mafanikio.

Alidai kuwa baadaye watu walisema kuna mtu katumbukia kisimani ndipo walipongozana na kuukuta mwili wake kisimani.

Katika kesi hiyo, Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili Alis Tomasi na Stev Mzava huku upande wa utetezi uliongozwa na Amosi Gahese.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo akiangalia handaki lililokuwa linatumiwa na wapigania uhuru wa nchi zilizo kusini mwa Afrika lililopo Wilaya ya Kongwa Mkoani Dodoma, kambi hiyo ilitumiwa na nchi za Msumbiji, Zimbabwe, Botswana, Afrika ya Kusini na Namibia. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Gari linalohusishwa lapelekwa mahakamani

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imepokea kielelezo cha gari aina ya Landrover lenye namba za usajili T 429 BYY kinachohusishwa katika mauji ya mdogo wa marehemu Erasto Msuya, maarufu Bilionea Msuya, Aneth Msuya, baada ya gari hilo kuhifadhiwa kwa zaidi ya miaka sita katika Kituo cha Polisi Chang'ombe.

Washitakiwa katika kesi hiyo ya mauji ni aliyekuwa mke wa bilionea huyo, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela (40). Aneth aliuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Uamuzi huo umetolewa na Jaji Edwin Kakolaki wa mahakama hiyo baada ya kupitilia mbali pingamizi la awali lililotolewa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala kwa madai kuwa gari hilo halikuwapo kwenye orodha ya vielelezo ambavyo washtakiwa walisomewa awali.

Jaji Kakolaki alisema kwa kutafakari maelezo ya pande zote mbili, sheria na kesi iliyohusika, mahakama inaona kuwa katika mambo mengi yaliyotajwa hayabishaniwi kuwa kielelezo kilichokusudiwa kutolewa Mahakama Kuu, lazima kiwe kimesomwa katika mahakama ya chini.

Alidai kuwa madhumuni ya kukiweka katika orodha kielelezo ni ili washtakiwa wawe na ufahamu kujua ushahidi ambao utakuwa mbele yao, basi pale panapokuwapo na kusahaulika kwa kielelezo, mhusika anatakiwa kuthibitisha katika kifungu namba 289(1)(4) cha CPA.

"Katika shauri hili, hakuna ubishi kwamba Kibatala alipewa taarifa ya kuongezwa kwa kielelezo hicho na mahakama pia. Kwa hiyo, upande wa mashtaka umeweza kuthibitisha taarifa hiyo kwa kufuata sheria. Kwa hiyo, kielelezo hicho kinaweza kupokewa na mahakama," alisema.

Aliongeza kuwa hadi mahakama inafikia hatua hiyo, iliona taarifa iliyotolewa na upande wa mashitaka ilikidhi vigezo vya kisheria vya kuongeza kielelezo hicho.

Baada ya uamuzi huo, aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha mwaka 2016, George Katabazi aliomba mahakama ipokee gari hilo kama kielelezo wakati akitoa ushahidi wake jinsi alivyokamata gari hilo mkoani humo na kulileta Dar es Salaam kwa ajili ya upelelezi.

Katika pingamizi hilo, Kibatala alidai kuwa kielelezo hicho hakikuwapo wakati washtakiwa wanasomewa maelezo ya mashahidi na pia hajawahi kupewa taarifa na upande wa mashtaka kuwa wanataka kuongeza kielelezo hicho na wala mahakama haina taarifa hiyo.

Alidai katika shauri namba 523/2020 dhidi ya Saidi Malikita na Jamhuri, majaji wametoa masharti ya jinsi taarifa kama hiyo inatakiwa kutolewa chini ya kifungu namba 246(2) cha CPA Sura ya 20 kama iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Serikali Marietta Maguta, alidai kuwa walimpa taarifa Kibatala kuwa wanataka kuongeza kielelezo, lakini alikataa kupokea kwa madai kuwa hatokuwa na pingamizi, lakini baada ya Jaji kumbana, alikubali kupewa taarifa hiyo.

Katika maelezo ya onyo, Miriam anaeleza kuwa aliamua kumuua wifi yake kwa sababu alikuwa 'anamfuatafuata' katika suala la usimamizi wa mirathi ya mumewe, marehemu Bilionea Msuya na katika kutekeleza mauaji hayo, alimkodi mtu ambaye alimlipa Sh. milioni 20.

Maelezo hayo ya Miriam yalisomwa mahakamani hapo na shahidi wa kwanza wa upande wa mashtaka, WP Sajenti Mwajuma, aliyemhoji mshtakiwa huyo na kuandika maelezo yake alipotiwa mbaroni, baada ya maelezo hayo kupokewa mahakamani hapo kuwa kielelezo cha ushahidi wa upande wa mashtaka.

# TAMISEMI yamulika wanaokwamisha ujenzi wa shule za msingi

**Na James Mwanamyoto,** SINGIDA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, amesema ofisi yake haitosita kumchukulia hatua atakayebainika kukwamisha ujenzi wa shule za msingi na ukarabati wa madarasa.

Amesema tayari fedha za ujenzi na ukarabati huo zimetolewa na serikali ili kuboresha miundombinu ya elimu msingi. Ndejembi alitoa angalizo hilo mkoani Singida jana wakati wa ziara yake ya kikazi katika Manispaa ya Singida na Halmashauri ya Wilaya ya Singida iliyolenga kukagua utekelezaji wa ujenzi wa shule za msingi na ukarabati wa madarasa kupitia mradi wa BOOST unaosimamiwa na Ofisi ya Rais -TAMISEMI.

Alisisitiza kuwa watakaobainika kukwamisha mradi huo watachukuliwa hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine wenye nia ovu ya kukwamisha miradi yenye tija kwa wananchi na maendeleo ya taifa.

Ndejembi pia aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha wanakamilisha kwa wakati miradi yote ya ujenzi wa shule na ukarabati wa madarasa ili thamani ya fedha ionekane.

"Ninawaomba mshimwangushe Mheshimiwa Rais, hakikisheni mnakamilisha ujenzi ifikapo tarehe 30 Juni mwaka huu kama ilivyopangwa ili kumpa nguvu Mheshimiwa Rais kuleta fedha nyingine," aliagiza.

Ndejembi alisema serikali imetoa Sh. bilioni 230 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi na ujenzi wa shule mpya katika maeneo yenye uhitaji mkubwa nchini.

Aliitaja ni dhamira yake njema ya serikali kuhakikisha watoto wanapata elimu katika mazingira bora.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskasi Muragili, aliishukuru serikali kwa kuipatia wilaya yake Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi.

Ndejembi alihitimisha ziara yake ya kikazi katika Wilaya ya Manyoni mkoani Singida kwa kuwasisitiza wakurugenzi wote nchini na wakuu wa idara za elimu msingi na sekondari kuhakikisha wananunua vifaa vyote vya ujenzi vinavyohitajika kabla ya mwaka wa fedha kuisha ili miradi inayoendelea kutekelezwa ikamilike kwa wakati.

## TANGAZO

The Guardian www.ippmedia.com

The Home of Great Newspaper

# Our Regional Offices and Representatives




*Feel free to contact for:*

**ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS**

**HEAD OFFICE**

THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe @Nipashetz

The Guardian @Theguardiantz

IPPmedia.com

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunaunga mkono kufuta ada vyuo vya ufundi, michango imulikwe

**DHIMA** kuu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 hadi 2025 ni kupunguza walau nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025, yaani miaka miwili ijayo.

Katika kufanikisha hilo, serikali imekuwa na mikakati mingi, mmojawapo ni kuanzisha kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaotoka familia duni.

Mikopo hiyo ilianza kutolewa 1999, mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na miaka mitano baadaye, ilipotimu mwaka 2004, ikatungwa sheria ya kuanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) iliyopewa jukumu la kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kukusanya marejesho kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo toka mwaka 1999.

Huku kukitolewa wastani wa Sh. bilioni 600 kwa mwaka kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, serikali imependekeza kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati kuanzia mwaka ujao wa masomo.

Serikali pia imependekeza katika mwaka wa fedha 2023/24 kuondoa ada kwa wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne na kupangiwa kujiunga na vyuo vya ufundi.

Vyuo hivyo ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC).

Ni pendekezo lililotangazwa bungeni Alhamisi ya juma hili na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipowasilisha mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Aliitaja hatua hiyo inalenga kuongeza idadi ya wataalamu.

Ni hatua inayokwenda sambamba na pendekezo lingine la kuongeza kiwango cha posho ya kujikimu, maarufu boom, kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Sh. 8,500 hadi Sh. 10,000 kwa siku kuanzia mwaka ujao wa masomo.

Nipashe, tukiwa wadau wa elimu na wabia katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo inayofuata (2025-2050), tunaunga mkono mapendekezo hayo ya serikali.

Tunaamini uamuzi huo wa serikali utaongeza wataalam wenye ujuzi na elimu inayohitajika katika zama hizi za mapinduzi ya nne ya viwanda.

Ada katika maeneo tajwa imekuwa kikwazo kwa wanafunzi wengi wanaotoka katika familia zisizo na hali nzuri kiuchumi, hata baadhi yao kushindwa kuendelea na masomo.


Tunayaunga mkono mapendekezo hayo ya serikali kwa kuwa yamefanyika kipindi ambacho kuna mchakato wa mabadiliko ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, toleo la mwaka 2023 na mabadiliko ya mitaala yanayofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau kwa lengo la kutoa elimu ya amali kwa ngazi zote kuanzia shule za awali, itakayowanufaisha vijana kujiajiri au kuajiriwa na kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa.

Hata hivyo, Nipashe tunatoa rai kwa serikali kuendelea kuchukua hatua dhidi ya utitiri wa michango katika taasisi za elimu nchini, vinginevyo kufuta ada na kuanzisha programu ya mikopo kwa wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne hakutokuwa na maana.

Upo ushuhuda wa wanafunzi toka familia zenye kipato duni kushindwa kuendelea na masomo kutokana na si tu kukosa ada, bali fedha kwa ajili ya michango mingi iliyoko katika shule na vyuo nchini. Michango hii imulikwe kwa maslahi ya Taifa!

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tunapojadili jambo tuwe na uhakika, tusiwe wapotoshaji

**MAKUBALIANO** kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai ya uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam yameibua mjadala mkubwa katika jamii na kusababisha sintofahamu.

Sintofahamu hiyo inatokana na baadhi ya watu wanaojadili kutopitia vifungu vyote vya mkataba huo na kuvielewa, hali ambayo imeanza kuchanganya wananchi.

Katika mjadala huo, wapo wanaopinga uwezekaji huo na wengine kuukubali, huku kila upande ukiwa na sababu zake ambazo zinaufanya uupinge au kuukubali uwekezaji huo.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa uhuru kila Mtanzania kutoa maoni yake au kuhoji jambo ambalo anaona haliko sawa, bila kuwekewa mizengwe.

Lakini katika sakata hilo, ninadhani kuna umuhimu wa kuwa na akiba ya maneno, ili kuepuka kudhalilika baadaye pale ufafanuzi wa jambo lenyewe unapokuja kutolewa.

Kimsingi, sakata hilo linaendana na mambo ya kisheria, hivyo kwa mtu asiyejua sheria kama mimi sidhani kama atakuwa sahihi kujadili jambo ambalo hana utaalamu nalo na wala hajaona mkataba wenyewe.

Hapa ndipo ninapotaka kujikita zaidi, kwamba mtu hujasoma mkataba na pia si mtaalamu wa sheria, lakini unakubali kujadili jambo ambalo hulijui na matokeo yake ni kusababisha utapotoshaji.

Kwanza, ninaomba nieleweke kuwa sipingi mtu kutoa maoni, lakini pia ni vyema kutoa maoni katika jambo ambalo unalijua, ili kuisaidia jamii kuwa na uelewa kuhusu jambo linalojadiliwa.

Bila kuzingatia hilo, kitakachotokea ni upotoshaji ambao kwa namna moja au nyingine unawachanganya wananchi na kushindwa kuelewa ni wapi ukweli ulipo hasa kuhusu sakata hilo la kisheria.

Hayo ndio yanayoendelea katika sakata la makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na ya Dubai kuhusu uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, ambapo Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), imeingilia kati.

TPA imeamua kuingilia kati baada ya kubaini upotoshaji kuhusu makubaliano yaliyopo kati ya serikali hizo mbili ikiwa ni wiki chache tangu mjadala huo uanze kupamba moto.

Taarifa ya TPA inalekeza kuwa serikali haina mpango wa kuipa kampuni ya DP World ya Dubai kandarasi ya kuendesha Bandari ya Dar es Salaam kwa miaka 100.

Ikumbukwe kuwa suala la kutoa Bandari ya Dar es Salaam kwa mwekezaji kwa muda wa miaka 100 ndilo ambalo limejaa vichwani mwa Watanzania huku chanzo chake kikiwa ni mjadala huo.

Kama nilivyoeleza awali, mjadala huo mpana ulihusisha watu wa kada mbalimbali wakiwamo wataalamu wa sheria, wasio wataalamu, wanasiasa na wengine ambao ninadhani watakuwa wamejadili kitu wasichokijua.

Hata kama Katiba inaruhusu kutoa maoni, lakini vyema kutojadili jambo la kusikia. Ni vyema kuliona kwanza na kujipa muda wa kulitafakari kabla ya kulitolea maoni kama njia ya kuwa na akiba ya maneno.

Kwa mujibu wa TPA, Azimio la Bunge linalohusu mkataba ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaingia na Serikali ya Dubai ukomo wake ni miezi 12 kwa ajili ya kutoa nafasi kwa serikali hizo mbili kushirikiana katika uboreshaji wa bandari.

Lakini pia kwa mujibu wa TPA, makubaliano ya uendeshaji wa bandari hayahusu bandari zote za Tanzania kama inavyojadiliwa, bali ni sehemu tu ya Bandari ya Dar es Salaam.

TPA inafafanua kuwa uendelezaji huo utaongeza ufanisi wa upakuaji makasha kutoka siku tano hadi saa 24. Pia ushirikiano wa nchi hizo mbili unalenga kukuza ajira za Watanzania na kufungua fursa za kiuchumi na kijamii kupitia uwekezaji katika baadhi ya maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam, maeneo huru ya kiuchumi, viwanda na mnyororo wa usafirishaji kwenda nchi jirani.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, naye anafafanua serikali imeichagua kampuni ya kimataifa ya huduma za bandari ya Dubai Port World (DPW) kutoka Dubai kwa lengo la kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa asilimia 233.7 katika kipindi cha miaka 10 ijayo.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Watanzania tupunguze kelele, Rais Samia anastahili pongezi



Pascal Mayalla

LEO ninaendelea na mada ya wiki iliyopita kuhusu makubaliano ya kiserikali, IGA ambapo Bunge letu limeridhia makubaliano ya IGA kati ya serikali yetu na kampuni ya DPW ya Dubai kutuendeshea bandari ombalo ni jambo zuri, lakini kuna kelele nyingi za huku na kule.

Kelele nyingine ni za kushangaza kwa watu kutokujua IGA ni nini na HGA ni nini. Sasa kwa vile na mimi mwandishi wako wa makala hizi pia ni mwanasheria na wakili wa kujitegemea, ninaomba kujitolea kuelimisha umma kidogo kuhusu IGA na HGA kwa kuwasisitiza Watanzania tupunguze kelele, kupotosha na kulaumu kwenye hili la bandari.

Rais Samia anastahili pongezi za dhati na sio lawama! IGA na DPW ni makubaliano tu, siyo mkataba.

Mkataba ni HGA! Kabla ya kwenda huko tuanze na jambo kuu la kwanza la msingi kabisa ni utendaji wa bandari zetu na uwezo wetu wa uendeshaji, ni mdogo, hivyo tunahitaji usaidizi.

Jambo la pili kubwa na la msingi sana ni nia njema ya dhati na dhamira safi ya Rais wetu Samia kulisaidia taifa letu kutoka hapa tulipo, tusonge mbele kimaendeleo na kufika kule tulikopaswa kuwa. Maadam Mama Samia ana nia njema na dhamira safi, ninaomba tuendelee kumuunga mkono kwa dhati ili kutimiza nia hiyo.

Ila katika utekelezaji nia njema hiyo, ndipo kwenye matatizo, kuanzia matatizo makubwa ya msingi ya kisheria, hadi matatizo madogo madogo ya uelewa finyu na tafsiri potofu za hapa na pale, ambayo hayamhusu kabisa Rais Samia, lakini kwa vile mkubwa ni jalala, kila kitu anatupiwa yeye!

Wakati matatizo mengine wala hayamhusu kabisa yeye kama Samia, ila kwa vile yeye ndio kichwa cha nchi, ndio nembo yetu, hawezi kukwepa kuhusishwa na kutajwatajwa mara hivi mara vile.

Nichukue fursa hii kuendelea kumpongeza Rais wetu Mama Samia kwa kuendelea kuwa na ngozi ngumu! Maana kuna vitu vinasemwa, ukijiuliza kama angekuwa ni Magufuli, vingesemwa? Hata huo mkataba wa IGA tungeuona? Hata huko bungeni ungepelekwa?

Mnyonge tumnyongeni jamani, haki yake mpeni! Kwenye hili la kupeleka mkataba huu wa IGA kuridhiwa na Bunge, ni jambo jema linalostahili pongezi za dhati.

Sasa tuje kwenye hili la IGA na HGA. Hapa Watanzania wanahitaji kuelimishwa hii IGA ni nini na HGA ni nini?

IGA ni neno la Kiingereza linaloitwa Inter Governmental Agreement.

Ni makubaliano kati ya nchi na nchi. Siyo mkataba wa utekelezaji wa kazi. Ni mkataba wa makubaliano kati ya serikali yetu na serikali ya Dubai kuingia mkataba wa kimataifa wa ushirikiano.

Mkataba wenyewe wa ushirikiano ndio unaitwa HGA, yaani Host Government Agreement, huu ndio mkataba. Kila mkataba ni makubaliano ila sio kila makubaliano ni mkataba.

Kitu kilichojadiliwa na kuridhiwa na Bunge letu ni IGA na siyo HGA, hivyo hata ikithibitika pasipo shaka kuwa kuna mambo hayajakaa sawa kwenye makubaliano hayo ya IGA, mambo hayo yatarekebishwa kabla ya kuingia mkataba wa HGA na serikali yetu, hivyo Tanzania kufaidika kwa kuboreshewa bandari zetu na mwekezaji DPW kufaidika kwa kuvuna mapato halali kwa uwekezaji wake, hivyo wote wawili kufaidika kwa kufikia hali inayoitwa 'a win win situation' na Tanzania kama nchi kufaidika.

Japo serikali yetu ina watendaji wazuri wa kusimamia maslahi ya taifa, lakini huku nje mitaani kuna kuwa watu wazuri wenye uwezo mkubwa wa kuisaidia nchi yetu na serikali yetu pengine kuliko hata hao waliopo serikalini, hoja za watu hawa zisikilizwe na kutathminiwa kama zina manufaa zijumuishwe ili tupate mkataba mzuri wa HGA.

Hivyo, nimalizie kwa kutoa wito, kila mwenye uelewa na ushauri mzuri wa kusaidia, ajitokeze, atoe ushauri wa namna bora ya kuiboresha HGA inayokuja na kuiomba serikali yetu iwe sikivu kupokea michango chanya, tutaisaidia sana serikali yetu, tutamsaidia sana Rais wetu Samia na kulisaidia taifa letu Tanzania.

Ninaendelea kusisitiza Rais wetu, Mama Samia, ana nia njema ya kweli na ya dhati kulisaidia taifa letu, tumuunge mkono tukiwamo sisi watu wa mhimili wa nne, vyombo vya habari, tuna wajibu wa kulisaidia taifa letu kwa kuhabarisha taarifa sahihi na kuelimisha maeneo yenye ukakasi kwenye hii IGA ili hivyo vipengele kakasi vya IGA viboreshwe kwenye HGA ili hii kazi nzuri ya Mama Samia iendelee!

Kwa vile Rais Samia ana nia njema ya dhati kuisaidia nchi yetu, wasaidizi wake na sisi Watanzania wengine wote tuna wajibu wa kumsaidia na kulisaidia taifa letu na huu ndio uzalendo wa kweli.

**0754270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania kwa pamoja tukatae makanisa sampuli hii



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WATANZANIA tuanze kujiuliza tunakokwenda au tunakoelekea kimaisha sasa, kwani tutaishia kuchanganyikiwa na kujikuta njiapanda na maisha kutukwamia.

Hivi sasa tunasikia kuibuka makanisa kibao karibu kila kona ya nchi ambako kuna watu wanajinasibu kujipa uchungaji na uaskofu, wakirubuni watu na 'kuwapiga' fedha.

Hivi karibuni baada ya saga la Zumaridi aliyeibuka na kujitamkia kuwa alikuwa mbinguni ambako alikutana na Mungu, sasa limeibuka kanisa lingine Misungwi, Mwanza, linalojinasibu kutibu watu bila kwenda hospitalini.

Endapo wasingeibuka watoa taarifa na kuwafumbua macho viongozi kuhusu kuwapo kanisa la aina hiyo, bila shaka roho za watu zingepotea kama lile la Malindi, Kenya, ambako watu walidanganywa wasile ili wafe hatimaye wakakutane na Yesu.

Utajiuliza kwanini mambo haya yanatokea, lakini unaweza kujijibu kuwa ni kutokana na ugumu wa maisha, na pia watu kutoaminiana au kutoamini taasisi zilizopo kuwahudumia na hivyo kuamua vinginevyo.

Hali ya maisha ni ngumu, hivyo ili mtu apate matibabu sharti aingie mfukoni, akikosa hivyo basi atahamia ambako hatakiwi kuingia mfukoni kwa kina kirefu, ambako ni kanisani atakakotoa sadaka pia.

Ni watu ambao wanaona ugumu kupata bima ya afya bila kipato kitokanacho na ajira au biashara, hivyo unakwama na unapougua basi utasubiri umauti wako, kwani unakuwa haumo kati ya wanaoweza kutibiwa ndani na nje ya nchi.

Wachungaji na maaskofu hao 'wa mchongo', hutumia fursa hiyo kurubuni watu wakiwafungia mahali wakisingizia kuwaombea na kuwaaminisha, kuwa karibu na Mungu, na matokeo yake hawaponi bali kujikuta wamepoteza maisha.

Watu zaidi ya 300 waliorubuniwa wakagoma kula hatimaye kufariki dunia huko Shakahola, Kenya, hawakutoa funzo kwa wenzetu wa Misungwi kwenye Kanisa la Lulembo ambako wanazuiwa na wanandoa wawili wakiwatoza fedha na kuwapa maeneo kujijengea wodi zao.

Wanandoa hawa wanapoulizwa, wanasema, 'sisi hatutoi huduma ya matibabu bali maombezi' na ikishindikana, huwatuma hospitalini kwa matibabu.

Wanamdanganya nani wakati wanawagawia maeneo kujenga nyumba za kuishi, kuna nafasi tena ya kwenda hospitalini hapo?

Wanageuza hilo kanisa kuwa hospitali, huku watu wakipoteza maisha hapo, bila kutambuliwa. Kuna tofauti gani na Shakahola? Hivi kwanini viongozi wanashindwa kung'amua utapeli huu mpaka kufikia hatua hiyo?

Hivi kweli, Mbunge wa Misungwi hakuwa anajua kuwapo kanisa hilo? Au alijua lakini kulinda kura zake mwaka 2025 akiogopa kuudhi wapigakura? Tabia kama hii ndiyo inayogharimu maisha ya wenzetu kwa ujinga wao tu.

Watanzania tumekuwa hivi siku zote, hususan wanasiasa, ambao wamekuwa wakilea uovu kisiasa wakichelea kukosa kura kwenye uchaguzi mkuu. Hili limejibainisha kwa madereva wa bodaoda, wamachinga na sasa waumini wa makanisa.

Hakuna watu wanaovunja sheria za barabarani na kusababisha ajali na vifo na ulemavu wa kudumu kama madereva wa bodaboda, lakini wanapokabiliwa na mkono wa sheria, utasikia vijana wanajitafutia riziki, tena wapunguziwe hata adhabu, na kubatizwa majina ya maofisa usafirishaji!

Machinga wakikiuka sheria, zikiwamo za kutumika kukwepa kodi, utasikia 'waacheni wajasiriamali hao wanajitafutia', na kuendeleza vurugu wakipambana na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Wamiliki wa baa nao wakikiuka sheria za uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa kupiga kelele kwenye kumbi zao, wakifungiwa biashara zao kwa makosa hayo, utasikia wanasiasa wanaibuka na kukemea na hata kuwafungulia wakidai eti uchumi unaathirika!

Sasa tunashuhudia makanisa yakiibuka kama uyoga, kila kona ya nchi, wanaibuka wachungaji na maaskofu wa mchongo kila mahali, wananchi wanatumia ugumu wa maisha yao kujiunga huko na kuibiwa, huku pia wakiathirika kiafya.

Viongozi wapo wanaangalia, wakisubiri litokee la kutokea ndipo wainuke na kuungana na Rais kutoa salamu za pole kwa waliofikwa na majanga na kurudi kuendelea na maisha kama kawaida.

Tumejifunza nini kutoka kwa Zumaridi? Tunajifuza nini kutokana na Kanisa la Shakahola, Kenya? Kama hatujifunzi, basi litakuja la kututokea na kutustaajabisha na sisi kuwa funzo kwa mataifa mengine.

Hivi kweli, Watanzania tunahitaji utitiri wa makanisa yasiyoeleweka kama hili la Misungwi na mengine yaliyopo ambayo pengine viongozi hawajayaona au wanasali huko? Hivi msajili wa makanisa hukagua majengo anayosajili kama nyumba za ibada kujua nini yanafanyza?

Kama msajili na kwa mamlaka yake, amezunguka nchini na kujiridhisha kuwapo au kutokuwapo kwa makanisa kama hayo ili kuhalalisha nafasi yake serikalini? Kama sivyo anasubiri nini kupisha asaidiwe?

Makanisa yasiyokidhi mahitaji yafutwe na hakuna Mungu wa makanisa kama hayo, atakayeshuka na kuhoji kwanini yamefungwa, kutofanya hivyo ni kuendelea kuhalalisha uovu na kuhatarisha maisha ya watu na ya siku Mungu wa kweli atatuona!

**Alamsiki!**

# Kijana ajikata shingo kwa mashine ya mbao

**Na Mary Mosha ,**
MOSHI

MWITA Warioba anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 35 na 40, mkazi wa Kiusa, fundi seremala, amefariki dunia akidaiwa kujiua kwenye mashine ya kuchania mbao kwa kujikata shingo.

Akizungumzia tukio hilo, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Yahya Mdogo, alisema lilitokea Juni 16 mwaka huu asubuhi huko Mtaa wa Rau katika kiwanda cha kuchana mbao wilayani Moshi.

"Kabla ya tukio hilo, kijana huyo alikuwa ameajiriwa katika karakana hiyo kabla ya kusimamishwa kazi kwa tuhuma za wizi wa fedha za mapato ya karakana hiyo na kutakiwa kutoa ufafanuzi kuhusu fedha hizo.

"Aliamua kuchukua hatua hiyo ya kujikata shingo kwenye mashine inayozungushwa kwa umeme kwa makusudi.

"Aliacha ujumbe unaosomeka kuwa ameamua kwa hiari yake kujiua. Mwili wake umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini KCMC," alisema Kaimu Kamanda Mdogo.

Baadhi ya wananchi wanaoishi karibu na karakana hiyo, akiwamo Filbert Mushi, waliutaja uamuzi aliouchukua kijana huyo ni mbaya na kuiomba serikali kuona namna ya kutoa elimu kwa jamii.

"Kutokana na ugumu wa maisha, vijana wengi wanakabiliwa na matatizo ya afya ya akili. Serikali itafute namna mzuri ya kutoa elimu ya mara kwa mara.

"Pia waajiri kuweni makini wakati wa utatuzi wa migogoro. Hekima iongezeke kutokana na hali ilivyo kwa sasa," alishauri Edna Ngasa.

# Tanzania yatekeleza mradi kuleta suluhu soko la ajira

**Na Romana Mallya**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi sita zinazotekeleza mradi wa awamu ya tatu (CFIT III) wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), ukijikita kuleta suluhu la soko la ajira kwa wahitimu vyuo vikuu.

Mradi huo unalenga kuangalia mitaala ya elimu ya juu ili itoe ujuzi kwa wanafunzi kwa kuwa wabunifu, kujiajiri na kuangalia namna wanavyokwenda pamoja na mabadiliko ya dunia.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Kitengo cha Elimu UNESCO, Tanzania, Faith Shayo, wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ukikutanisha nchi sita zinazoutekeleza.

Nchi nyingine ni Cote d'lvoire, Ethiopia, Gabon, Senegal na Uganda.

Alisema UNESCO inaratibu mradi huo ukiwa ni awamu ya tatu ukijikita kwenye elimu ya juu hususani eneo la elimu ya ufundi.

Alisema lengo kubwa la mradi huo ni kuboresha ubora wa utoaji wa elimu ya juu hasa kuangalia changamoto zilizopo kwenye soko la ajira kwa kuwa, wanafunzi wanaopohitimu hukutana na tatizo hilo.

"Mradi huu ukiwa umefadhiliwa na Serikali ya Watu wa China, ukitekelezwa na UNESCO katika nchi sita,

Tanzania ikiwamo, umejikita kunufaisha vyuo vikuu viwili katika kila nchi. Kwa Tanzania vyuo vilivyopo ni UDSM na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST)," alisema.

Shayo alisema mradi huo unajikita kwenda kuleta suluhu kwenye soko la ajira kwa kuangalia mitaala ya elimu ya juu ili itoe ujuzi kwa wanafunzi kwa kuwa wabunifu, kujiajiri na kuangalia namna wanavyokwenda pamoja na mabadiliko ya dunia.

Alisema kila mwaka mradi huo huwa na mkutano mkuu wa mwaka na kwamba, walianza mwaka 2021 na wanategemea kuumaliza mwezi Desemba, mwakani.

"Kwa mwaka huu, Tanzania imechaguliwa kuandaa mkutano huu na tunashukuru UDSM kwa kutuandalia mkutano, tuna wageni kutoka nchi tano," alisema.

Pia alisema uhusiano kati ya vyuo vikuu, serikali pamoja na sekta binafsi utatengeneza mitaala bora kwa kuwa sekta hiyo ndiyo waajiri wakubwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Prof. Carolyne Nombo, kupitia hotuba yake iliyosomwa na Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema vyuo vikuu vinahitaji rasilimali watu bora na miundombinu ya kufundishia na utafiti.

Alisema mradi huo wenye lengo la kuongeza uwezo wa taasisi za elimu ya juu ili kukabiliana na mahitaji ya kitaifa ya rasilimali watu inayohitajika umekuja muda muafaka.

alisema kila nchi inayotekeleza mradi huo inatarajia kuona matokeo ikiwamo ubora na umuhimu wa mtaala na programu zilizoboreshwa ambazo zinakidhi mahitaji ya soko la ajira, kuongeza ushirikishwaji na kukuza usawa wa kijinsia.

Balozi wa China nchini, CHEN Mingjian, alisema lengo la mradi huo ni kuongeza uwezo wa taasisi za elimu ya juu kukabiliana na mahitaji ya ujuzi kwa maendeleo ya taifa kwa kuwezesha ushirikiano kati ya taasisi hizo na sekta ya viwanda.

Mwakilishi wa UNESCO Tanzania, Michael Toto, alisema, "Ninachukua nafasi hii kusisitiza jitihada za UNESCO na kujitolea kwa dhati kukuza elimu kwa maendeleo endelevu na kusukuma mbele ajenda ya elimu 2030 kwa ujumla wake."



Aliyekuwa Katibu Tawala Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Desderia Haule (kushoto) akimkabidhi rasmi ofisi hiyo Katibu Tawala mpya, Mohamed Mussa Mfaki (kulia) ambapo makabidhiano hayo yamefanyika rasmi katika Ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Muheza katika kijiji cha Lusanga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mgodi Buzwagi kugeuzwa viwanda

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amesema eneo la machimbo ya dhahabu la Buzwagi wilayani Kahama mkoani humo ambako shughuli za uchimbaji madini zimesitishwa, litakuwa la uwekezaji.

Amesema kwa sasa eneo hilo litaitwa Samia Special Economic Zone na kutajenga viwanda vingi, hivyo mkoa unakaribisha wawekezaji. Aliyasema hayo juzi alipozungumza na viongozi wa dini, wazee maarufu na machifu mkoani humo. Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 612.3 kwa mkoa huo ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Christina alisema mkoa huo unaendelea kutafuta wawekezaji katika eneo lililokuwa linatumika katika shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu la Buzwagi ambalo sasa ni la uwekezaji.

"Eneo za zaidi ya hekta 1,333 ambazo zilikuwa zinatumiwa na Mgodi wa Buzwagi kuchimba madini ya dhahabu. Tumeligeuza kuwa kitovu cha uchumi, litaitwa 'Samia Special Economic zone' na vitajengwa viwanda vingi na tunakaribisha wawekezaji," alisema Mkuu wa Mkoa alisema hivi karibuni akiwa na viongozi wengine wa Wilaya ya Kahama, walitembelea Falme za Kiarabu katika eneo la Dubai Textile City kujifunza na kukaribisha wawekezaji waje kuwekeza na amepanga kukutana na wafanyabiashara mkoani humo ili nao wachangamkie fursa hiyo.

Alisema serikali pia imeshatenga zaidi ya ekari 2,000 kwa ajili ya kujengwa Bandari Kavu (Dry Port) ambayo itaendelea kuchagiza ukuaji wa uchumi wa mkoa na kukarabati viwanja vya ndege. Katika hatua nyingine, kiongozi huyo wa mkoa aliwataka viongozi wa dini, wazee maarufu na machifu mkoani humo, kumuunga mkono Rais Samia katika uwekezaji wa bandari ambao umelenga kukuza uchumi wananchi na kuwataka wapuuze maneno ya upotoshaji.

Katika tamko lao la pamoja lilisomwa na Chifu Charles Njange Jidola, kundi hilo lilimpongeza Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi mkoani humo ili kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kundi hilo pia lililoaani na kupinga vikali watu lililowaita wanapotosha jamii kuhusu uwekezaji wa bandari.

# MAISHA

JUNI 18, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 14




## FURAHIA KEKI YA KAROTI

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Usijenge nyumba kwenye udongo wa mfinyanzi




## KATUNIKA


Ukurasa 16



## MIDOMO MURUA

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




SHINYANGA

MARA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| P | | P | A | N | D | E |
| A | | | | E | | N |
| M | | B | E | E | | D |
| B | A | O | | M | I | E |
| A | | N | I | A | | L |
| N | | D | | | | E |
| A | M | A | N | A | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


NAE, ALE, KOO, GUU, UPEPO, ABEBE, EZEKA, AUNGE, ONDOSHA, PUNGUZA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

KATIKA VIVULI HIVI VITATU, KIVULI KIMOJA TU KINAFANANA NA KISHADA, KITAFUTE



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

JAMAA mmoja ambaye ni mara ya kwanza kutembelea mjini, aliwaacha watu hoi kwa kicheko baada ya kupelekwa katika kibanda cha kununulia koni.

**Mama:** Ebu nipatie koni mbili ya kwangu na huyu ndugu yangu

**Jamaa:** Duu, chakula gani hiki mbona kama konokono wa kule shambani, ila huyu ana rangi nzuri

**Mama:** Hapana hii ni koni

**Jamaa:** Tafadhali mama siwezi kula, bora uninunulie togwa

**Mama:** Sema taratibu unanitia aibu.

**SWALI**

Tabia za binadamu zinakaribiana na mnyama gani wa porini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Kinachowapata wanawake wenye dharau kwa wakwe

KARIBU msomaji wangu, leo tunaendeleza mada iliyopita kuhusu wakwe. Nilitaja mambo kadhaa ambayo mke anapaswa kujua kuhusu wakwe. Nikasema ipo misingi na kanuni ambazo tunapaswa kuzingatia ili maisha yawe mazuri na tulivu.

Ndoa nyingi zinapata misukosuko mingi kwa sababu tu wanandoa wenyewe wanakiuka misingi hiyo. Wanawake wengi leo wapo katika sintofahamu nyingi kuhusu ndoa zao. Wengine wamezikimbia, wengine wamejitia nguvu kutegemeana na yale wanayopitia. Wengine wamepoteza maisha kwa sababu tu hawakuzingatia mambo ya msingi.

Leo msomaji wangu nikazie eneo moja nililotaja na kuahidi kutoa mifano hai, kinamama waliopuuzia wazazi au ndugu wa mume na kupata madhara. Tambua kuwa mume wako ana wazazi wake.

Wanawake wengi wanapoingia katika ndoa, hupuuzia sana eneo hili ndio maana wanapata madhara makubwa katika maisha. Wake wengi huwa wanaishi kana kwamba waume zao walitoka mbinguni na hawana wazazi, huku wao wakiwahudumia wazazi wao.

Hii ni hatari sana! Kama ukishindwa kutambua kuwa mume wako ana wazazi na ndugu zake, na sehemu kubwa bado wanamtegemea, hautoishi kwa utulivu hakika! Ukiwadharau, wanaweza kufikia hatua ya kukutoa katika nyumba ya mtoto wao! Uwe na hekima ya kuwapenda, usiwabague.

Hata kama wazazi hawa wamekufanyia ubaya wa aina gani, mume wako anatarajia uendelee kuwapenda, sawa na vile unavyowapenda wazazi wako. Hebu sikia habari hii ya kusikitisha ikiwa ni madhara ya kudharau wakwe. Usithubutu kuua kuku aliyetaga dhahabu!

Yupo mama mmoja alisimulia tukio lililompata mama, rafiki yake aliyepoteza maisha miaka kadhaa iliyopita, chanzo kikitokana na kuwadharau wakwe na ndugu wengine wa mume wake.

Wanawake hawa wawili wote wameolewa kwa ndoa nzuri na pia wanaume zao wana kazi nzuri katika taasisi kubwa serikalini. Kingine kinachoshabihiana kwao ni waume zao wanatoka mkoa mmoja na kabila moja.

Mama huyu akisimulia mazingira ya kifo cha rafiki yake, akasema kuwa kabla ya kifo alikuwa akimshirikisha mambo mbalimbali anayokutana nayo katika maisha yake ya ndoa. Tayari Mungu alishamjalia watoto wawili, nao walikuwa bado wadogo, mmoja miaka minne na mwingine miaka miwili.

Dada huyu pale alipokuwa anatembelewa na mama mkwe au mawifi alikuwa hapendi. Alikuwa haonyeshi ukarimu, ni kama vile anawaona mzigo nyumbani kwake. Hata kupika alikuwa akiwalazimisha wajipikie na kuwaonea kinyaa hadi waondoke.

Vituko kama hivi viliwaudhi sana ndugu wa mume ikiwamo wazazi wake. Dada huyu akasahau kuwa hawa ni wazazi na ndugu wa mumewe na bado wana wajibu wa kumtembelea kuwajulia hali na kupata misaada midogo midogo. Pia alipaswa kufahamu wakwe zake wanamchunguza, wanamfuatilia.

Vituko vilipozidi, upande wa wakwe wakaona kuwa bibie hawapendi na ndipo wakapanga njama ya kumnyamazisha. Unajua ushirikina bado upo sana katika baadhi ya familia hasa za vijijini.

Siku moja akatumwa wifi toka kijijini kuja kuweka kambi pale nyumbani kwa kaka yake. Mara nyingi mume wa bibie huyu yupo nje ya mkoa kikazi. Dada yake akavizia kaka yupo safarini akaja na kukaa siku kadhaa na wifi yake.

Kumbe alikuja na dawa wanazojua wao. Lengo kumchanganya bibie. Alipomaliza kazi yake, wifi akaondoka. Miezi miwili baadaye bibie akaanza kuumwa vitu visivyoeleweka. Akienda hospitalini madaktari wanasema hawaoni ugonjwa japokuwa walimpatia dawa za kutuliza maumivu.

Miezi mitatu baadaye, bibie huyu alipoteza maisha na kumwachia mumewe watoto wadogo. Ama kweli Maisha ndivyo Yalivyo. Mama huyu mwingine naye akasema yaliyompata rafiki yake yafaa kuyatafakari sana.

Naye ana viashiria vya tatizo kama la rafiki yake. Amekuwa haonyeshi changamko anapotembelewa na wakwe au mawifi zake. Hata mama mkwe anapompigia simu kumwomba fedha kidogo za matumizi kijijini humjibu hana japokuwa kiuhalisia anazo. Mumewe anasomesha baadhi ya watoto wa ndugu zake, jambo ambalo halipendi kabisa. Je, wakwe na ndugu wengine wa mume wakimfanyizia mabaya atamlaumu nani?

Kuwa mwangalifu na jitahidi kutunza nyumba yako kwani wao wanatafuta makosa yako. Usiwape nafasi kukukosoa. Wapende, wavumilie kwani pia ipo siku utakuwa mama mkwe. Wiki ijayo nitakumbushia zaidi uhusiano kati ya mke na mama mkwe, ndoa nyingi zipone! ***Una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Tozo mpya za saruji zitachochea mfumuko wa bei

KODI ndio uhai wa Taifa. Serikali imependekeza kuongezwa tozo ya ushuru katika saruji kuanzia mwaka ujao wa fedha (2023/24).

Ni jambo zuri kuwa na chanzo cha mapato kama hiki na vinginevyo, kwa kuwa lengo lake ni kuliwezesha Taifa kupata mapato yake yatakayotumika kuendesha maendeleo ya nchi yetu.

Pasi na shaka nchi yoyote duniani inandeshwa kwa kodi inazokusanya. Hata bila kuwa mchumi, unaweza ukaona ni jinsi gani kodi ina nafasi muhimu katika kujenga uchumi imara na unaojitegemea.

Ndio! Ngoja nianzie hapa. Kama Bunge litapitisha pendekezo hilo bila kutazama kwa namna gani ongezeko la ushuru kwenye saruji litakavyokuwa na athari, litatengeneza shida katika vifaa vya ujenzi, badala ya kuleta unafuu kwa wananchi. Bei itakuwa juu.

Mwenendo wa mfumuko wa bei katika vifaa vya ujenzi, bila shaka unaweza kuwa usioelezeka. Kuongeza ushuru wa saruji, utawafanya wanyonge kuwa na mwaka mchungu, huenda kusiwe na shida kwa wenye nazo.

Ninaona mwenendo wa mfumuko wa bei (gharama za maisha) utazidi kupaa na hali ya maisha ya watu itakuwa mbaya zaidi kama alivyotahadhirisha juzi Profesa wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Humphrey Mushi.

Tangu mapendekezo ya bajeti ya serikali yaliposomwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, bungeni Alhamisi, kuna maswali nimekuwa ninajiuliza.

Mojawapo ni kwanini serikali isiondoe kodi katika vifaa vya ujenzi ili kuwezesha wananchi kujenga nyumba bora?

Ni rai yangu kwa serikali kulitizama upya jambo hili la kuongezwa ushuru katika saruji na kuachana na mpango huu.

Ninatamani kuona serikali ikiweka mikakati ya kuhami maisha ya watu na kujiandaa kukabiliana na hali hiyo na kuwaandaa kuongeza uzalishaji na angalau kukidhi mahitaji ya ndani.

Ni vyema serikali ijielekeze kubuni vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kugharamia bajeti yake badala ya kuongeza tozo na ushuru katika saruji.

Mwenendo wa uchumi na hali ya maisha ya watu inafahamika. Kilio cha wananchi ni kuwapo mfumuko wa bei za bidhaa muhimu, jambo ambalo limekuwa likisababisha kupanda kwa gharama za maisha.

Tumeshuhudia machungu ya kupanda kwa bei za mafuta ya petroli na dizeli nchini kutokana na changamoto zinazoikumba dunia kwa sasa kama vita vinavyoendelea huko kwa wenzetu.

Kuna bidhaa kama vile vyakula (mahindi, maharage, ngano, sukari na mchele) vimepanda zaidi ndani ya mwaka mmoja.

Kupanda kwa vifaa vya ujenzi kama vile saruji, mabati na nondo kumeshuhudiwa pia. Bado wananchi hawajatulia, wanaugulia maumivu ya mfumuko huo wa bei mitaani.

Katika hali hiyo, ninafikiri hakuna haja kwa serikali yetu kuongeza tozo katika bidhaa muhimu kama saruji. Uamuzi utaathiri maisha ya watu.

Mwaka mmoja uliopita, Watanzania walianza kupata faraja baada ya kusikia UDSM wamebuni saruji mbadala, itakayomwezesha mnunuzi kupunguza karibu nusu ya gharama.

Wenzetu hao wa UDSM walituambia kwamba teknolojia hiyo inakuja wakati bei ya mfuko mmoja wa saruji wa kilogramu 50 unauzwa Sh. 17,000 kutoka Sh. 14,500 ya mwaka juzi, huku tofali moja likiuzwa Sh. 1,500 badala ya Sh. 1,200.

Wakati ule ninakumbuka alinukuliwa na vyombo vya habari, Mhadhiri Mwandamizi Dk. Aldo Kitalika, wakati wa maonyesho ya kitaifa ya ubunifu, sayansi na teknolojia, akisema saruji hiyo inaweza kutengeneza matofali, vigae na hata katika kujenga barabara. Waheshimiwa, kwanini tusifikirie kwanza kuelekeza nguvu kuzalisha saruji hiyo badala ya kuongeza tozo ya ushuru wa saruji? Mbona kama itaongeza mfumuko wa bei?

Pendekezo la serikali ni kutoza Sh. 20 kwa kila kilo ya saruji inayoingizwa kutoka nje na inayozalishwa ndani. Kwa lugha rahisi, serikali inakusudia kutoza Sh. 1,000 kwa kila mfuko wa Kg 50 wa saruji.

*Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. ***Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI







JE unajua vazi la kikoi linaweza kugeuzwa kuwa nguo nzuri ya maharusi? Katika picha ni baadhi ya nguo za harusi zilizobuniwa kwa kutumia kitambaa cha kikoi.





# MITINDO

Na Mary Geofrey







# KIPUPWE KIMEWADIA

## Pigilia hivi upendeze

KIPINDI cha kipupwe ambacho kinaambatana na baridi la wastani, ni wakati ambao mavazi mazito yanatumika na wengi.

Mara nyingi uchaguzi wa mavazi yanapelekea mtu kupendeza kama akichagua sahihi, lakini kipindi cha baridi uzito wa nguo unazingatiwa sana.

Hata hivyo, uchaguzi wa mavazi ni jambo muhimu linalozingatiwa kwani ukienda kinyume unaweza kupoteza mwonekano wako mzuri.

Je unataka kutoka vizuri katika kipindi hiki cha kipupwe? Basi zingatia mambo haya muhimu.

**CHAGUA RANGI**

Kwa kawaida nguo za rangi nyeusi zinafaa kwa watu wa aina zote, iwe jaketi au suti mtu anapovaa inamtoa bomba.

Unaweza kuvaa nguo za tangi nyeusi na ukachanganya shati jeupe, suriali nyeusi au bluu.

**USIVAE NGUO NYINGI**

Unashauriwa kuacha kuvaa nguo nyingi katika kupambana na baridi la wastani, tabia hii inachangia uchafu pamoja na kuharibu umbo la mtu husika.

Hakikisha unavaa nguo zinazokupatia nafasi ya kutembea bila tatizo, mwili wako unahitaji kufanya kazi bila usumbufu.



UREMBO

Na Mary Geofrey

# MIDOMO MURUA

## kipindi cha kipupwe



BAADHI ya watu wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la ukavu wa mdomo na kuwasababishia kukosa raha na kuwafanya washindwe kujiamini wakati wa baridi.

Katika kupambana na baridi la kipupwe unaweza kufanya yafuatayo kubaki kwenye hali nzuri na mwonekano wako.

**Kunywa maji**

Kwa kawaida wataalamu wanashauri binadamu anywe maji kulingana na uzito wa mwili wake, lakini ili kufanya midomo yako kulainika hakikisha unakunywa angalau glasi nane za maji kila siku ili kuboresha ngozi yako.

**Matunda, mboga za majani**

Matunda pia hususani yenye maji maji kama karoti, matango, nyanya na matikiti yanaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kukinga au kukabiliana na tatizo hili na kuimarisha afya ya ngozi yako kwa ujumla.

**Mafuta ya mgando (Vaseline)**

Paka mafuta ya mgando au samli katika midomo yako kila unapotaka kulala, hii itasaidia kufanya midomo yako iwe na unyevunyevu.

**Lipbam**

Hakikisha unatumia mafuta maalum za kupaka katika midomo yako hasa wakati wa baridi 'lipbam'. Tumia majani ya hiliki kusugua katika midomo yako hii itakusaidia kuzifanya ziwe laini zaidi.

**Mswaki**

Sugua ngozi ya midomo yako kwa kutumia mswaki na maji ya uvuvugu angalau mara moja kwa wiki, hii itasaidia kuondoa seli zilizokufa katika ngozi ya midomo yako.

**Limao na glycelin**

Paka mchanganyiko wa maji ya limao na 'glycelin' katika ngozi ya midomo yako kila usiku, acha kwa usiku mzima hadi asubuhi ndipo uoshe, hii itakusaidia kung'arisha midomo yako.

**Tui bubu la nazi**

Lainisha ngozi ya midomo yako kwa kupaka tui bubu la nazi katika midomo yako.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia keki ya karoti

MAPISHI ya keki nyumbani imekuwa jambo rahisi sana kwa sababu wengi wana vifaa vinavyoweza kutumika kupikia.

Mara nyingi tumezoea kupika keki za ladha tofauti lakini za karoti ni nadra kuziona, sasa leo tutaelekezana namna ya kupika.

**MAANDALIZI**

Mayai manne, siagi kikombe kimoja na robo, sukari nyeupe vikombe viwili, vanila vijiko viwili vya chai, unga vikombe viwili, baking powder vijiko viwili vya chai na chumvi nusu kijiko cha chai.

Mahitaji mengine ni cinnamon vijiko viwili vya chai, karoti gram 220, baking soda kijiko kimoja, nutmeg nusu kijiko cha chai, siagi ya maziwa robotatu kikombe na flaked coconut kikombe kimoja.

**Mahitaji**

Chukua bakuli weka unga, sukari, baking powder, baking soda, mdalasini, nutmeg, chumvi na nutmeg kisha changanya vizuri sana. Weka pembeni.

Chukua bakuli lingine weka mayai, butter, vanila na flaked coconut koroga mpaka viwe laini kabisa.

Mchanganyiko wenye mayai mwagia kwenye unga kisha koroga mpaka uone vimechanganyikana vizuri.

Chukua karoti ulizoziandaa ukazikwangua weka kwenye mchanganyiko ule wa keki.

Koroga vizuri sana.

Chukua chombo unachotumia kupikia keki yako kipake butter.

Chukua mchanganyiko wa keki mwagia kwenye chombo hicho, weka kwenye oven.

Washa oven weka nyuzi joto 350 F.

Dakika 45 zikipita, funua angalia kama keki imeiva. Chukua toothpick ichome katikati ya keki, kikitoka kikavu imeiva. Ikiwa bado irudishe kwenye oven.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## Ipambe sehemu ya kulia chakula kwa sinki zuri

**Na Restuta James**

SINKI la kunawia mikono linatajwa kuwa sehemu ya pambo katika eneo la kulia chakula. Hii ni kutokana na mwonekano na muundo wake.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Winnie Joseph, ameiambia NIPASHE katika mahojiano maalumu kwamba kumekuwa na miundo mipya ya kuvutia inayoendelea kuvumbuliwa na wana teknolojia.

Anasema katika sehemu ya chakula, imekuja miundo mipya kuanzia kwenye ramani ya ujenzi wa nyumba hadi nakshi zinazokamilisha eneo hilo.

Anasema moja ya pambo linaloongeza thamani na mwonekano wa eneo hilo ni sinki la kunawia mikono.

"Wavumbuzi wamekuja na muundo, mpya wa kisasa ambao unaleta uhalisia ndani ya nyumba. Sinki la kunawia la jiwe lililonakshiwa vizuri kama unavyoona," anasema Winnie, akionesha baadhi ya masinki hayo.

Anasema kitu pekee kinachovutia kwenye muundo huo ni utulivu unaoletwa na sinki hilo.

Winnie anasema masinki hayo yanapatikana kwa rangi tofauti tofauti ikiwamo nyeusi, kahawia na kijivu.

Hata hivyo, anasema muundo huo haujafuta yale ya udongo ambayo yanatumika hivi sasa kwani bado kuna watu wanaopendelea aina hiyo.

NIPASHE ambayo imetembelea maduka tofauti jijini Dar es Salaam, imebaini kuwa 'mchawi' wa aina hiyo mpya ya sinki ni bei kwani ni kubwa ikilinganishwa na ya udongo iliyozoeleka.

0753 333 330





# Usijenge nyumba kwenye udongo wa mfinyanzi

KUNA mambo mengi ambayo huchangia kuletha athari katika nyumba na hili tumekuwa tukijifunza kutokana na maelezo ya watalaamu mbalimbali wa sekta hiyo.

Watalaamu hao wamekuwa wanasema kwamba kama ilivyo kwa vitu vingine kukumbana na changamoto, uchaguzi wa eneo la ujenzi wa nyumba pia unahitaji umakini mkubwa.

Miongoni mwa vitu ambavyo vimekuwa vikisisitizwa na wataalamu hao ni kuzingatia au kuepuka kununua kiwanja na kujenga nyumba katika eneo ambalo linaweza kuleta athari kwa nyumba yako baadaye.

Na baadhi wamekuwa wanashauri kwamba japokuwa siyo utaratibu kwa watu wengi, lakini ni vyema na kwa usalama wa nyumba, kujenga utaratibu kabla ya kununua kiwanja kwa ajili ya matumizi ya ujenzi wa nyumba, ukawaona wataalamu wakakushauri kama ni salama au la.

Mtaalamu wa shughuli za ujenzi, Victor Mkalama anaeleza athari za kujenga nyumba kwenye kiwanja chenye udongo wa mfinyanzi.

Anaeleza kwamba udongo wa mfinyanzi una tabia ya kuvimba na kuongezeka ukubwa hasa unapopata maji na pia unapokauka husinyaa.

"Kwa maana hiyo udongo unapovimba na kuongezeka ukubwa, jengo hunyanyuliwa juu, lakini udongo unaposinyaa jengo hutitia,"anaelezea mtaalamu huyo.

"Kuna aina nyingi za udongo wa mfinyanzi na katika kila aina ya udongo huo hutofautiana na aina nyingine katika kuvimba au kusinyaa na hii inasababishwa na kiasi cha unyevunyevu kwenye ardhi husika," anasema.


Mtaalamu huyo anasema udongo huo wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo katika eneo husika linalotumika kujenga nyumba inapokatwa.

"Udongo hasa wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo inapokatwa, na hii inatokea kwa sababu mizizi hukomaa zaidi na kunyonya maji kwenye ardhi na kuchangia ongezeko la kiasi fulani cha unyevunyevu kwenye udongo huo,"anasema Mkalama.

"Na kuondolewa kwa maji katika udondo wa aina hiyo ya mfinyanzi kwa kunyonywa na mizizi ya miti husababisha udongo kuongezeka au kupungua ujazo kwa kiasi fulani hususani katika kipindi cha kiangazi au masika.

"Na kuvimba au kusinyaa huko kwa udongo ni hatari kwa msingi wa nyumba kwa sababu huchangia kuleta nyufa katika nyumba na wakati mwingine kuiharibu kabisa.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
HUYU MKINIACHA NAE NUSU SAA HAPA TULIPO NITAMCHAPA NGUMI HAJIELEWI
JUKWAANI
HUYU HATA MKINIACHA NAE HAPA MWAKA MZIMA ATABWABWAJA NA KUNIBWEKEA LAKINI HANG'ATI
WANA-SI - HASA
MUME WANGU TUONGEE KWA AMANI UMENIOA NIKIWA KIGOLI MPAKA SASA NIMEKONGO-LOKA SISIKII KUHUSU DENI LA MAHALI YANGU!
KABLA SIJAJIBU NAOMBA NISEME KUWA. NISIZIKWE HAPA MJINI ALAFU SIMAMIA KABURI LIJENGEWE
YULE DEMU CHAPOMBE WAKO NISHAMFIKISHA KWAKO NARUDI KUMALIZIA BIA YANGU
'UMEUA!' NAVYOMJUA MKE WANGU SIJUI KAMA ZIGO LA MAGENDO BADO LINAPUMUA
JAMANI MIMI NINA DAWA YA KUZINDIKA NDOA, KUZUIA MUME ASIENDE KWA HAWALA NA AKIENDA ASILALE, NA AKILALA ASIMPE HELA, NA AKIMPA HELA SIO ZOTE
ENZI ZANGU MTU HUYU NDUGUZE WANGEMZIKA WAMOTO!
UMEONA KITUONI NDIO SEHEMU SAHIHI YA KWENDA KUNISIFIA GONGO SITII MAJI?
POMBE HAINA ADABU!
SURA SINA HELA SINA MIPANGO SINA MKWARA SINA HATA 'AILAVYU' PIA SINA!
UMETIMULIWA KWA KUMPORO-MOSHEA MINENO MIBOVU DOKTA KISA NINI?
ETI SIRUHUSIWI 'KUNYWA' SABABU NITAHARIBU DOZI WAKATI NINA MWALIKO!
BWANA HARUSI MCHAGA... BI.HARUSI NI MUHAYA...HEBU PATA PICHA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIPEWA ACHA MASWALI MENGI

# Wanafunzi 40 wauawa, wengine watekwa nyara

**KAMPALA,** UGANDA

KAMANDA wa Jeshi la Uganda, (UPDF), Meja Jenerali, Dick Olum, amesema operesheni ya kuwaokoa wanafunzi waliotekwa nyara na waasi imeshika kasi.

Alisema kuwa wametuma ndege za kuwatafuta na kuwaokoa wanafunzi waliochukuliwa baada ya tukio la utekaji lililofanywa na waasi wa kundi la ADF.

Kulingana na kamanda huyo, baadhi ya wanafunzi, wengi wao wavulana waliteketezwa hadi kufa huku wasichana wakikatwakatwa na mapanga na wengine kuchukuliwa mateka.

Meja Oluma aliyasema hayo wakati akihutubia wakazi wa mji wa Kasese magharibi mwa Uganda baada ya tukio la kuuawa kwa wanafunzi 40 na wengine kujeruhiwa katika shambulio la kigaidi.

''Walikuja hapa wakalala siku mbili, ndio wakaja kuchoma watu, walitaka kuchoma magari ,wakaona magari ya jeshi wakarudi kwenye shule, sasa hivi tumetuma ndege kila sehemu inaenda kuwatafuta, tunataka kuokoa wale waliowateka wakaondoka nao'' alisema.

Jenerali Olum aliongeza kuwa waasi hao walifika katika eneo hilo la magharibi na kukaa kwa siku mbili kabla ya kufanya tukio.

"Tumepata habari kwamba waasi walikaa hapa kwa siku mbili kabla ya kuvamia shule, ndio wakahakikisha wanakuja wanafunga mlango kwa vijana, vijana walijaribu sana kupigana lakini walihakikisha wamechoma magodoro yao, nguvu ikawashinda, kwa wasichana walikuta mlango wazi, ndio wakaua na kuwakatakata'' alisisitiza Meja Jenerali Olum.

Shambulio dhidi ya shule hiyo ni tukio la kwanza la aina hiyo ndani ya Uganda kwa miaka mingi.

Mnamo 1998, waasi wa ADF walishambulia Taasisi ya Kiufundi ya Kichwamba wilayani Kabarole na kuwachoma moto wanafunzi 80 hadi kufa na kuwateka nyara zaidi ya 100.

Kundi la ADF liliundwa mashariki mwa Uganda katika miaka ya 1990 na kuanza vuguvugu dhidi ya Rais wa muda mrefu, Yoweri Museveni, kwa madai ya mateso ya serikali dhidi ya Waislamu.

Baada ya kushindwa na jeshi la Uganda mwaka 2001, lilihamia jimbo la Kivu Kaskazini nchini DRC.

Mwanzilishi mkuu wa kundi hilo, Jamil Makulu, alikamatwa nchini Tanzania mwaka 2015 na yuko kizuizini katika gereza la Uganda.

Waasi wa ADF wamekuwa wakiendesha shughuli zao kutoka ndani ya DRC kwa miongo miwili iliyopita.

**BBC**



Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, (katikati) akiwaongoza viongozi wa nchi nne za Afrika kutoka katika jengo la nchi hiyo baada ya kufanya mazungumzo ya kujaribu kusimamisha vita na Russia. **PICHA:BBC**

# Mali yaomba wanajeshi kuondolewa

**NEWYORK,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Mali ameutaka Umoja wa Mataifa kuondoa kikosi chake cha kulinda amani nchini humo mara moja.

Waziri Abdoulaye Diop, akihutubia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, alikishutumu kikosi hicho kinachofahamika kama Minusma, kwa kuwa sehemu ya tatizo katika kuchochea mivutano kati ya jumuiya.

Minusma ina zaidi ya askari 13,000, kwa muongo mmoja, vikosi hivyo vimeshindwa kukomesha kuenea kwa ghasia za wanajihadi.

Mamluki wa Wagner wa Russia sasa wanasaidia watawala wa kijeshi wa Mali.

Maofisa wa nchi za Magharibi wamemshutumu Wagner kwa ukiukaji wa haki za binadamu nchini Ukraine na baadhi ya maeneo ya Afrika, na mwezi uliopita Marekani ilitangaza vikwazo dhidi ya Ivan Maslov, ambaye ilimtaja kuwa Ofisa Mkuu wa Wagner nchini Mali.

Wagner haijazungumzia madai hayo ya Magharibi na shughuli zake nchini Mali na maeneo mengine ya Afrika bado zimegubikwa na usiri.

Ukosoaji wa Waziri Diop kwa Minusma ulifuatia pingamizi za awali za Mali kwa ushiriki wa muda mrefu wa Ufaransa nchini humo.

Diop alisema mgogoro wa kuaminiana kati ya mamlaka ya Mali na Minusma utamalizika na endapo kikosi hicho kitajiondoa bila kuchelewa nchini mwake.

Muda wa kuhudumu nchini humo kwa Minusma unatarajiwa kumalizika Juni 29, lakini mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres amependekeza ujumbe huo upitiwe upya kuzingatia vipaumbele vichache.

Umoja wa Mataifa kwa sasa unaorodhesha kikosi cha kijeshi kutoka Chad, Bangladesh na Misri kama kikosi kikubwa zaidi katika eneo hilo.

Ripoti ya kamishna mkuu wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa ilishutumu wanajeshi wa Mali na wanausalama wa kigeni kwa kuwaua zaidi ya watu 500 wakati wa operesheni katika kijiji cha Moura, katikati ya Mali, mwezi Machi mwaka jana.

**BBC**

## Viongozi Afrika kukutana na Putin

**MOSCOW,** RUSSIA

UJUMBE wa ngazi za juu wa Afrika unataraji kukutana na rais wa Russia Vladimir Putin, siku moja baada ya rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky kupuuza mwito wa mazungumzo kati ya nchi hizo mbili.

Timu hiyo ya kidiplomasia ilikuwa Ukraine juzi Ijumaa na kuelezea mashaka yanayolikumba bara la Afrika kutokana na uvamizi wa Russia nchini humo, na hasa kupanda kwa bei za nafaka, huku rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini akisisitizia umuhimu wa amani kwa njia ya mazungumzo.

Hata hivyo Zelensky aliondoa uwezekano huo katika mkutano pamoja na waandishi wa habari na kurudia matamshi aliyoyatoa mara kadhaa kwamba kuingia makubaliano na Russia kwa sasa kutamaanisha kusitisha kwa muda wa vita, mateso na machungu.

Zelensky badala yake ameliomba kundi hilo linalohusisha marais wanne kutoa mitizamo yao juu ya namna ya kumaliza uhalifu uliofanywa na Russia na kushughulikia suala la upatikanaji wa chakula cha kutosha.

**DW**

## Wahamiaji 104 waokolewa majini

**ATHENS,** UGIRIKI

SHUGHULI ya kuwatafuta walionusurika kwenye ajali ya boti iliyokuwa inawasafirisha wahamiaji katika bahari ya Mediterania imekamilika jana.

Walinzi wa pwani ya Ugiriki walikuwa wanaendelea na msako katika eneo hilo wakitumia manowari ya kijeshi, boti tatu za doria na helikopta, ingawa upepo mkali umekuwa ukizorotesha shughuli hiyo.

Matumaini ya kuwaokoa manusura zaidi ni kama yamepotea, baada ya boti hiyo ya uvuvi iliyokuwa imebeba wahamiaji kati ya 500 hadi 700 iliyokuwa ikitokea Afrika kwenda Ulaya kuzama siku ya Jumatano.

Jumla ya wahamiaji 104 waliokolewa na maiti 78 zilipatikana katika operesheni hiyo.

**DW**

# ‘Hali ya Mtoto wa Afrika bado mbaya’

**Na Beatrice Shayo**

WADAU wamesema hali ya Mtoto wa Afrika bado siyo nzuri huku baadhi ya watoto wakiishi katika mazingira magumu na wengine kuacha shule.

Mratibu Msaidizi wa Programu za Kielimu wa Shirika la Sote Pamoja katika Utu (ATD), Gasper Mbwambo, alitoa kauli hiyo wakati wa maadhimisho ya kilele Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo hufanyika kila Juni 16.

Katika maadhimisho hayo mwaka huu, Ubalozi wa Ufaransa na Ireland umefadhili wadau ambao walikutana Tandale katika kuadhimisha siku hiyo wakiwa na kaulimbiu ya ‘usafi na haki ya mazingira safi na salama kwa ukuaji wa watoto wa Dar es Salaam’.

“Tukizungumza mazingira gani huyo Mtoto wa Afrika yupo katika makundi mawili jamii ambayo tunaishi sisi sote kuna wale ambao wapo katika umaskini uliokidhiri vipi kuhusu mustakabari wa watoto wao kupata huduma ya shule, afya na malazi?” alihoji.

Mratibu huyo alisema familia ambazo wanafanya nazo kazi zina maisha duni na zina vijana wengi wenye umri wa kuanzia miaka 10 hadi 15, wengi wao ni wanaacha shule.

“Juzi nilikuwa ninazungumza na mwalimu mkuu wa shule moja, kuna kijana ameacha shule kwa sababu ya utoro lakini mwalimu naye hafahamu sababu za ndani.

“Ilibidi nimwelezee huyo kijana ameacha shule kutokana na hali duni ya maisha yao. Kuna mahitaji ya kimsingi anatakiwa kuyapata kama mtoto mwingine, huyu anayakosa kwa sababu mama ndiye mtafutaji na kipato anachokipata ni chini ya dola moja na baba wa kijana huyo ni mgonjwa, hawezi kujishughulisha na chochote,”alisema.

Mratibu huyo alisema kuwa katika maisha kama hayo, mtoto anakuwa ni mwathirika wa mwisho, hivyo upatikanaji wa huduma kwa baadhi ya watoto kulingana na utofauti wao katika makundi ya jamii ni tofauti.

Alisema usalama katika ulimwengu wa kidigitali nao ni changamoto kwa kuwa watoto wana uwezo wa kupata kila kitu katika mitandao.

Alisema kuwa mbaya zaidi bado hawajaweka ukomo wa baadhi ya maudhui ambayo mtoto hapaswi kuyaona, hali inayosababisha kubadilika kimaadili.

“Mtoto wa Afrika siwezi kusema yupo salama, nimetolea mfano wa mtoto mmoja lakini nyuma yake wapo wengi anawawakilisha, wapo wengine huko mikoani,” alisema.

Winfrida Noel, mwanafunzi wa darasa sita ambaye ni mshiriki wa maktaba ya mtaa kwa muda wa miaka mitatu Tandale, alipongeza serikali kwa kukemea vitendo vya ukatili kwa watoto kuanzia ngazi ya kitongoji hadi kitaifa.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mambo mazuri kwa watoto ikiwamo kuruhusu kuwarejesha shuleni waliopata ujauzito kuendelea na masomo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Pakacha, Kassimu Omary, alisema wameadhimisha siku hiyo kwa kushiriki upandaji wa miti, akisisitiza jamii ina haki ya kuhakikisha inamlinda mtoto na siyo kumfanyia vitendo viovu.

# Chongolo aonya uuzaji mashamba inakopita miradi ya umwagiliaji

**Na Ibrahim Joseph,** MPWAPWA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewatahadharisha wananchi wanaoishi jirani na miradi ya umwagiliaji, kuacha kuuza mashamba yao kwa wageni kwa kuwa maeneo hayo ni muhimu kwa ustawi wa maisha yao.

Chongolo alitoa tahadhari hiyo jana alipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Msagali wilayani Mpwapwa katika mwendelezo wa ziara yake mkoani Dodoma.

Katibu Mkuu huyo aliwataka wananchi wa maeneo hayo yaliyo karibu na miradi hiyo ya umwagiliaji kuacha kuuza mashamba yao kwa sababu miradi itakapokalika itawanufaisha kiuchumi. “Ndugu zangu wa Kijiji cha Ng’ambi na wananchi wengine walio jirani na miradi hii ya umwagiliaji, ninawaomba msiuze mashamba yenu. Neema inakuja hapa. Miradi hii itakapokamilika itakuwa na manufaa kwenu.

“Nimesikia kuna wageni wameanza kununua mashamba kwa wenyeji hapa, msikubali kuuza ardhi. Ni heri kuingia mkataba na mtu kuliko kuuza eneo lako,” alitoa angalizo.

Chongolo pia alisema miradi hiyo itakuwa ukombozi kwa wananchi hao kwa kuwa kilimo kitafanyika kwa mwaka mzima bila kutegemea mvua.

Mhandisi Nuru Simkoko alisema mradi wa umwagiliaji Msagali unajengwa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo na utagharimu Sh. bilioni 27.9 na unatarajiwa kutoa huduma ya maji katika hekta 3,500.

Alisema lengo la serikali ni kuwainua kiuchumi vijana na kinamama watakaopata eneo hilo kupitia mradi wa kilimo biashara (BBT) pamoja na wenyeji wa maeneo yaliyopo katika miradi.

Katika ziara yake hiyo, Chongolo pia aliagiza kuboreshwa na kutunzwa kwa eneo la kambi ya walipokuwa wanaishi wapigania uhuru wa nchi za kusini mwa Afrika lililoko Kongwa mkoani hapa.

Alisema eneo hilo lina historia kubwa ya ukombozi wa Bara la Afrika, hivyo linatakiwa kutunzwa kwa ajili ya historia ya vizazi vijavyo na wageni wanaofika nchini kulitembelea.

Alisema zipo nchi zilizohifadhi maeneo ya kihistoria kama China na Japan. Zinayatumia kuingiza fedha nyingi za kigeni kutokana na utalii.

Kambi hiyo waliishi wapigania uhuru wa nchi za Zimbambwe, Msumbiji, Afrika Kusini, Namibia na Botswana.

Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai alisema serikali haijaliendeleza eneo hilo la historia la Kongwa kama wanavyofanya kwa kambi ya Mazimbu mkoani Morogoro.

Ndugai alisema kuwa mwaka jana walifika mabalozi kutoka nchi ambazo walikaa wapigania uhuru wao na kuahidi kushirikiana na serikali kuliboresha eneo hilo.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# ‘Nikipita waninyooshea vidole, kisa sijakijua’



**Na Adam Fungamwango**

HILI nitakaloliandika hapa nadhani hakuna mwanadamu ambaye hajapitia. Ni kwamba unaweza kuchukiwa na watu wanaokujua na wasiokujua bila sababu yoyote.

Unaweza ukapita tu sehemu ukakuta tu kundi la watu ambao hawakujui, lakini kwa sababu wanazozijua wenyewe wakaanza kukuchukia bila sababu. Na ukipita wanaanza kukunyooshea vidole, kukusema na kukusengenya kana kwamba wanakufahamu ulikotokea, unapoishi na unaishi vipi.

Haya ni maisha ambayo wanadamu wengi wamepitia. Na kwa kweli inauma sana kuona huna ubaya na mtu, hujawahi hata kusalimiana nao, lakini wanatokea kukuchukia bila sababu.

Unaweza ukapita wanaanza kukucheka, hata ukawa hujui wanakucheka kwa sababu zipi. Pia inawezekana ukapita wakakaa kimya tu na kununa mpaka upite, wakaanza kusema.

Sasa usiombee ndiyo wakawa wamepata angalau taarifa zako kutoka kwa mtu anayekufahamu, hata kama za uongo, ndiyo utakoma.

Tena mtu huyo azilete kwa namna ya kukuponda, ipo siku unaweza kusikia hata wanaongea mafumbo juu ya jambo ambalo wewe unalifahamu na ukashtuka na kujiuliza wamejuaje. Hayo kwa upande wa watu ambao hawakufahamu vizuri.

Wapo ambao wanakufahamu. Baadhi yao wana tabia kama hizo. Wao wanachotaka kuona unaharibikiwa tu, kutetereka kimaisha ili wakucheke na kukuteta vizuri. Hapa utasengenywa vizuri sana, halafu unaweza ukavikwa kilemba cha ukoka, kama vile wanakusifia, au kukutia moyo hivi, lakini kinyume chake ukiondoka wataangua vicheko na kufurahia anguko lako na mapito unayopitia. Ila hawa hawawezi kukufanyia kitu kingine kibaya zaidi ya hicho.

Sasa iwe kinyume chake. Wawe wanakufahamu kuwa umetoka kwenye mazingira mabovu, lakini kila siku zinavyozidi kusonga mbele unafanikiwa.

Hapa binadamu wananuna. Wanachonuna huwa hakijulikani kwa sababu wao si watoaji. Mtoaji ni Mungu, alikunyima, lakini sasa ameamua kukupa.

Siku zote Mungu hakupi huzuni ya milele na raha ya wakati wote. Kuna wakati wa kulia na kucheka, wakati wa furaha na huzuni, kama vile ilivyo masika na kiangazi, jua na mvua, mchana na usiku.

Baadhi ya binadamu hutaka waone wenzao wanaharibikiwa kila kukicha.

Hiyo wao inawapa raha tu. Ukifanikiwa wananuna na kukuchukia. Watasema mengi, kuwa unaringa, unajiona, na ukishawaona watu wa aina hiyo kuwa makini, inakuwa ni hatari sana na wanaweza kukufanyia chochote kile ili uharibikiwe, udhurike ili warudishe furaha yao.

Kama nilivyosema afadhali ukiwa huna kitu, watakachofurahia ni kukucheka na kukuteta, lakini ukianza kufanikiwa wanakuwa na chuki inayoambatana na roho mbaya, na hapo inabidi uwe na tahadhari.

Mwanamuziki Eddy Sheggy, aliyefariki mwaka 2000, akiwa na bendi ya Washirika Tanzania Stars, alitunga wimbo aliouita ‘Kisa’.

Analalamika jinsi anavyotetwa na jirani zake kwa sababu ya mafanikio yake. Jina lake limekuwa kama wimbo midomoni mwao, mchana kutwa wanamkalia kikao tu.

Anasema kisa hakijui kwa sababu hajala cha mtu, chochote alichonacho ni juhudi, bidii yake na vingine ni vya urithi tu.

**Tuangalie mashairi ya wimbo huu.**

*“Ni jambo la kushangaza Sheggy kanitangazia ubaya kwa watu eee, kuniharibia jina langu mimi ooo, nami sina ubaya na yeye ooo, najiuliza ee.*

*Jina langu ni kama wimbo midomoni mwao, hawaishi kulitajataja mchana kutwa, nikipita waninyooshea vidole mama ee, kisa ee, hicho kisa sijakijua eee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Jina langu ni kama wimbo midomoni mwao, hawaishi kulitajataja mchana kutwa, nikipita waninyooshea vidole mama ee, kisa ee, hicho kisa sijakijua eee. Kisa hicho kisa, sijakijua ee.*

*Kisa eee mama, kisa sijajua. Kisa eee sherry, kisa niseme nini ee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Nyumba niliyonayo mimi eee, bidii yangu baba, nimejenga ee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Gari nililonalo mimi eee, bidii yangu baba, nimenunua ee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Shamba nililonalo mimi eee, urithi wangu baba, kaniachia mama ee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Kisa yoyoyo, kisa sijajua nifanye nini yoyo. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Kisa yoyoyo, kisa sijajua jamani eee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Kisa wowo mama ee, kisa wowowo nini eee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Kisa wowo mama ee, kisa wowowo nini eee. Kisa hicho kisa, sijakijua.*

*Kisa wowo mama ee, kisa wowowo nini eee. Kisa hicho kisa, sijakijua.”*

Hawa ndiyo binadamu walivyo na hii ndiyo dunia. Wanacheka jino pembe moyoni wanasononeka, wema ni hao na wabaya ni hao hao, amini usiamini kukuchekea siyo kufurahi nawe. Binadamu madhilumu, ana vituko vya sumu kushinda ya nyoka, si wazuri binadamu usione wanacheka.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-15

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




AKASHUSHA pumzi kidogo na kutoa kikohozi chepesi. Ilionekana sasa siyo pati tena, bali kumegeuka kuwa na kikao cha kifamilia.

"Wakaniuliza tutampataje huyo aliyekupigia simu, nikawaambia yupo tu pale mtaani kwetu na namfahamu. Wakaniomba niwapeleke. Kwa bahati nzuri niwaambie tu ugomvi wangu na yeye umekwisha, alivyopata na yeye mchumba akaja kuniomba radhi, siku si nyingi na yeye ataolewa.

Nikawapeleka kwake, tukayazungumza, tukakubaliana na ndiyo Belo akaandaa huu mpango wa pati hii ili kupata fursa ya sisi kuueleza hapa kila mtu aelewe na wasioamini waamini. Mimi nimemaliza ya kwangu."

Belo akasimama, akamkaribisha mwanamke mwingine. Huyu ndiye aliyepiga simu kumchamba Pendo, lakini simu tayari alikuwa ameshabadilishiwa, ipo kwa Husna."

Aliyesimama ni msichana aliyeonekana kuwa na umri wa miaka 22 mpaka 25 hivi. Alikuwa mrefu, maji ya kunde. Mdomo wake ulikuwa mpana kidogo. Pamoja na wembamba wake, alikuwa na umbile la kuvutia namba nane.

Alivaa nguo za kumetameta kwa ajili ya shughuli hiyo. Alisimama huku akiona aibu, ambayo ilimfanya atabasamu, halafu ainamishe kichwa chini.

"Habari zenu mabibi na mabwana, tuko hapa kwenye sherehe zetu za leo kwa mambo mawili. Kwanza ni 'bethdei' ya mtoto wetu, halafu haya ambayo yamejitokeza.

Mimi sitosema mengi sana, kwa sababu waliopita wameongea karibuni yote. Ila mimi nitasema mambo machache na lengo ni kujenga.

Kujenga ndipo kumesababisha sisi kufika hapa. Kama alivyosema mwenzangu Pendo, mimi ndiye niliyepiga simu siku ile na nilimpigia Pendo.

Unajua tena wakati ule mambo yalivyokuwa mwenyewe amesema hapa, sitaki kurudia. Tukapatana na kukawa marafiki, baadaye wakaja mababa hawa wawili pamoja na Pendo nyumbani kwangu, wakanieleza kuwa simu niliyopiga siku ile na kumuambia maneno yale ilipokelewa na mwanamke mwingine kwa sababu simu zilibadilishwa kwa fundi, sasa aliyepokea kawaka kwa mumewe, anataka amuambie huyo hawara ni nani, akaamua kuondoka nyumbani.

Sasa wanataka sisi wote wawili tukathibitishe na siku hiyo kutakuwa na 'bethdei' nyumbani kwa mmoja wapo na watakuja kutuchukua," Akasema kwa sauti iliyojaa aibu, lakini akiwa hamuangalii mtu usoni.

**Sasa wanataka sisi wote wawili tukathibitishe na siku hiyo kutakuwa na 'bethdei' nyumbani kwa mmoja wapo na watakuja kutuchukua," Akasema kwa sauti iliyojaa aibu, lakini akiwa hamuangalii mtu usoni. Kulikuwa na minong'ono ukumbini hapo, yakamfikia, akaangua kicheko na kupaza sauti.**

Kulikuwa na minong'ono ukumbini hapo, yakamfikia, akaangua kicheko na kupaza sauti.

"Naitwa Zawadi," alijibu na hii ilitokana na kupata minong'ono kuwa hajawatajia watu jina lake.

"Tukashauriana na mwenzangu tukaona bora tukubali kwa sababu sisi ndiyo tumelizua na ugomvi wetu. Mbona sisi tumepatana? Sasa kwa nini mtu ambaye alipata ujumbe huo akadhani ni wake, akaondoka kwenye ndoa yake, tusikubali apatane na mumewe? Tukaamua tuje, tuweke ushahidi wetu hapa ili mwenzetu aamini, kwa sababu ni kweli kabisa, bila hivi hata kama mimi siwezi kuamini.

Sijamfahamu tu hapa ni yupi, lakini namuomba radhi na naomba na yeye aje hapa ili apokee radhi, halafu atuambie kwa hili mwenzetu ameamua vipi, lakini nadhani tu yatakuwa yameisha." Akamaliza na kuketi.

Belo alisimama tena, safari hii akimkaribisha shemeji yake.

"Sasa kwa namna ya pekee, nimkaribishe shemeji yangu, mke wa mdogo wangu, Dan.

Kwa taarifa tu wale wasiyomhafamu, yeye ndiye aliyebadilishiwa simu akachukua ya Pendo, ya kwake akapewa Pendo, fundi Massawe apochanganya madawa." Maneno yake yalisababisha baadhi ya watu waangue kicheko.

Kusimama kwake Husna kulisababisha watu wapige makofi. Hakuwa mbali sana na kina Pendo. Akamtazama kwa chati Zawadi, akili yake ikarejesha kumbukumbu nyuma ya maneno ambayo siku hiyo aliyasikia, akamuumiza. Na akaumia kweli kiasi cha kumchukia mumewe, ndugu zake na ndoa pia.

"Enheee ndiyo wewe nilikuwa nakutaka shoga a'ngu. Nilikuwa nakutafuta haswa.

Mwanamke usiokuwa na haya, usiojua kupendeza sketi, blauzi, dela, suruali wala kijora.

Bibi wewe hupendezi sokoni wala 'super market,' mwanamke usioujua wanja, shedo wala lipstick, saluni wewe kwako kituo cha polisi, tulia hivyo hivyo wewe kama unanyolewa, utanieleza nini wewe, yaani umeing'ang'ania ndoa hadi umeipata, sasa sikiliza huwezi kukaa kwa raha na huyo mwanaume wakati mimi nipo hai.

Mimi ndiyo ilikuwa niolewe na huyo mwanaume, unamfanyia dawa, unamlisha limbwata, kaniacha, kaja kukuoa, sasa mimi na wewe, nakula na wewe sahani moja na hii ndoa haina tena miezi mitatu nahakikisha inasambaratika..."

Akaikumbuka sauti hiyo kama vile ilikuwa inazungumza jana, kumbe inakaribia mwezi wa tatu sasa.

"Yamekuingia ee, pole sana. Sasa nachokwambia ni hiki, hivi sasa huyo bwana unayeringia ninaye miye.

Usishangae, ninaye hapa ndani hivi navyokueleza, najua anaoga nini, anakula nini, na anavaa vipi, ulidhani ukiolewa bwana atakuwa wa kwako peke yako eee, huyu hapa dada.

Au nikupe simu uongee naye, hahahaha, utakufa kwa presha bure sikupi.

Yaani umeolewa lakini bwana kaja kwangu, lo. Mwamke gani usiyojua kumlea mwanaume, mwanamke usiyejua kumnyeyekea bwana, mwanamke usiyojua mahaba, tena ninavyokwambia bwana ninaye miye, bwana yumo ndani anajilia vyake..."

Leo amemuona laivu mwanamke aliyekuwa akimtolea maneno yale yaliyomchoma akachomeka. Huyo ndiye aliyedhania kuwa ni mke mwenzake.

"Mhh! Mbona hafanani? Mwanamke ana maneno mabovu hivi." Akajiambia mwenyewe. Lakini hapo hapo akajikumbusha kuwa ilikuwa ni zamu yake na yeye kuongea.

Tena yeye ndiye anasubiriwa kuwa mwamuzi wa kisa kizima na mbinu iliyofanywa na Belo pamoja na Massawe kuwakutanisha hapo kwenye sherehe.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# GIGY KUNA MARAFIKI NA WANAFIKI

UNAAMBIWA msanii wa bongo fleva, Gigy Money, amejikuta mnyonge baada ya mastaa wakubwa kususia sherehe yake ya kuzaliwa.

Katika sherehe hiyo mastaa watano pekee ndio waliofika kujumuika naye kati ya idadi kubwa ya wasanii waliopewa mwaliko wa kwenda kuhudhuria.

Sherehe hiyo ilifanyika Tips Coco jijini Dar es Salaam, lakini jambo la kushangaza msanii huyo machachari na mwenye kujitolea katika matukio mbalimbali ya wasanii wenzake, alijikuta akiwa mpweke kutokana na mastaa wenzake kuonekana kama kumsusia.

Waliohudhuria sherehe hiyo ni Nandy, Amber Lulu , Msami na Chino, Petit Man na Masha Love.

@el_mando_tz anasema kuwa Gigy aliwaalika wasanii wengi sana lakini hawakutokea na tukio hilo ndio kipimo cha namna wasanii wetu walivyo hawana ushirikiano na upendo kwa wao wenyewe.



# PEPO AU LAANA?



UNAWEZA kusema kwamba pepo mbaya anazidi kumwandama mchekeshaji maarufu duniani, William Henry Cosby Jr (85), baada ya wanawake wengine tisa kumlalamikia kuwafanyia unyanyasaji wa kijinsia.

Mchekeshaji huyo kutoka Marekani, ambaye kipindi chake cha The Cosby Show, kimepata umaarufu kwa miongo kadhaa, anadaiwa kutumia nguvu, umaarufu wake na heshima kuwadhulumu.

Kesi hiyo imewasilishwa Jumatano katika mahakama ya shirikisho huko Nevada, inadaiwa kuwa wanawake hao walinyweshwa dawa za kulevya na kushambuliwa kingono kati ya 1979 na 1992 katika nyumba zake zilizopo Las Vegas, Reno na Lake Tahoe, kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na hoteli.

Mwanamke mmoja pia amedai kuwa Cosby, alikuwa kaimu mshauri wake, alimrubuni kutoka New York hadi Nevada, ambako alimnywesha kinywaji chenye kilevi kwenye chumba cha hoteli na kisha kumbaka.

Nyota huyo mwenye umri mkubwa ameshutumiwa kwa ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia kwa zaidi ya wanawake 60 hadi sasa.

Hata hivyo mwenyewe anakanusha madai yote yanayohusu uhalifu wa ngono.

Cosby alihukumiwa na kukaa kifungo cha jela kwa miaka mitatu katika gereza la serikali karibu na Philadelphia kabla ya mahakama ya juu kutupilia mbali hukumu hiyo na kumwachilia huru mnamo 2021.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**WALKER AWINDWA**

KLABU ya Bayern Munich inajadili kumnunua beki wa Manchester City na England, Kyle Walker mwenye umri wa miaka 33. (*Mail*)

**JACKSON SAFI CHELSEA**

CHELSEA imekubaliana maslahi binafsi na mshambuliaji wa Villarreal na Senegal, Nicolas Jackson mwenye umri wa miaka 21 ambaye ana kipengele cha kuachiliwa cha euro milioni 35. (*The Athletic*)

**RAMOS ATAKIWA MAN**

KLABU ya Manchester United inapewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Ureno mwenye thamani ya pauni milioni 80, Goncalo Ramos mwenye umri wa miaka 21 kutoka Benfica. (*Sun*)

**HAVERTZ ANUKIA ARSENAL**

CHELSEA imekataa ofa ya awali kutoka kwa Arsenal kwa mchezaji Kai Havertz lakini mazungumzo yanaendelea na mshambuliaji huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 24. (*Telegraph*)

**MAN NAYO YAMTAKA**

KLABU ya Bayern Munich sasa wamejiunga na Arsenal katika mbio za kumsajili Kai Havertz. (*Sky Sport*)

**GUNDOGAN AKARIBIA BARCA**

BARCELONA imempa Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 32 kipaumbele katika usajili wao msimu huu na wamezidisha kumsaka kiungo huyo wa kati wa Ujerumani, ambaye mkataba wake unamalizika Manchester City, kwa kumpa mkataba bora wa miaka mitatu. ((*Athletic*)

**DE GEA KUONDOKA**

DAVID de Gea mwenye umri wa miaka 31 anatazamiwa kuondoka Manchester United msimu huu, huku mazungumzo ya mkataba na mlinda mlango huyo wa Hispania pale Old Trafford "yakionekana kuwa mabaya". (*Mirror)*

**KULUSEVSKI KUBAKI SPURS**

WINGA wa Sweden, Dejan Kulusevski mwenye umri wa miaka 23 atabadilisha uhamisho wake wa mkopo kutoka Juventus kwenda Tottenham Hotspur kuwa uhamisho wa kudumu baada ya klabu hizo mbili kukubaliana ada ya pauni milioni 25.6. (*90min*)

**KOVASIC KUTUA CITY**

KLABU ya Manchester City iko ukingoni kukamilisha dili la takribani pauni milioni 34 kumsajili kiungo wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic mwenye umri wa miaka 29, kutoka Chelsea. (*ESPN*)

**CAICEDO AWINDWA CHELSEA**

KLABU ya Brighton inatafuta malipo ya kima cha pauni milioni 100 kutoka Chelsea kwa kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21. (*Athletic*)

**SILVA ATAKIWA PSG**

KLABU ya Paris St-Germain ina nia ya kumsajili Bernardo Silva na wameanza mazungumzo na wakala wa winga huyo wa Ureno, lakini Manchester City hawataki kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. (*Nicolo Schira*)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI: NASUBIRI KWA HAMU KUANZA KUCHEZA MAREKANI

**NEW YORK,** Marekani

### ●●● Asema yupo tayari kwa changamoto mpya Marekani...

LIONEL Messi amesema anahamu ya kuanza sura inayofuata ya maisha yake atakapohamia Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MSL, baada ya kushindwa kujiunga na Barcelona kama alivyotarajia.

**Messi mwenye umri wa miaka 35 alitangaza wiki iliyopita uamuzi wake wa kujiunga na Inter Miami CF mara tu mkataba wake na Paris Saint-Germain utakapokamilika Juni 30 na akasema yuko tayari kwa changamoto inayomsubiri nchini Marekani.**

"Niko sawa," aliiambia TV Publica ya Argentina. "Hapo awali, tulikuwa na wazo tofauti (kurejea Barcelona).

"Tuna furaha na uamuzi tuliochukua. Niko tayari na nina shauku ya kukabiliana na changamoto hii mpya, mabadiliko haya."

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia la 2022 akiwa na Argentina, Messi alikuwa na ofa za kurejea klabu yake ya zamani Barcelona na vile vile uwezekano wa kuhamia klabu ya Al Hilal ya Saudi Arabia, lakini hatimaye aliamua kujiunga na mmiliki mwenza David Beckham pale Inter Miami katika MLS.

"Uamuzi huo ulikuwa hatua muhimu lakini wakati huo huo, nilikuwa najua maana yake, kuhusu kile nilichokuwa nikifanya," Messi aliongeza. "Tuna furaha."

Messi, ambaye alifichua wiki hii hana mpango wa kucheza Kombe la Dunia 2026, hapunguzi kasi.

Nahodha huyo wa Argentina alifunga bao la haraka zaidi katika soka lake la kimataifa, akifunga bao baada ya sekunde 79 wakati walipoilaza Australia 2-0 katika mechi ya kirafiki siku ya Alhamisi.


"Kama ninasema mkweli, kama hatungeshinda Kombe la Dunia, nisingekuwa tena nachezea timu ya taifa," alisema Messi.

"Siwezi kuiacha timu ya taifa kama bingwa wa dunia. Nataka kufurahia hili."

Messi alikuwa amepoteza fainali tatu mfululizo akiwa na Argentina kabla ya kubeba Copa America mwaka wa 2021 baada ya kuwashinda wapinzani wao Brazil katika fainali.

Hakuna mchezaji aliyekuwa na presha zaidi kuelekea Kombe la Dunia nchini Qatar kuliko Messi.

"Sikulia lakini niliteseka sana. Nilikuwa na wakati mgumu sana, lakini siku zote nilikuwa na hamu ya kushinda kitu nikiwa na timu ya taifa. Nilijua akilini mwangu kwamba ningefanikisha."



# Greenwood ajumuishwa kikosi cha Man United

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imemjumuisha Mason Greenwood kwenye orodha yao ya kikosi kwa ajili ya msimu wa 2023-24, klabu hiyo ilitangaza Ijumaa, lakini vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United bado haijafanya uamuzi juu ya mustakabali wa mchezaji huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amesimamishwa kucheza mechi na mazoezi tangu aliposhtakiwa kwa jaribio la ubakaji, kushambulia Januari 2022 - mashtaka ambayo yalifutwa Februari 2023.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba kujumuishwa kwa Greenwood kwenye orodha ya klabu iliyobaki, ambayo imetumwa kwenye Ligi Kuu, inaonesha nafasi yake kama mchezaji aliye na mkataba na haizingatiwi kuwa kiashirio cha mustakabali wake United.

Ana mkataba Old Trafford hadi mwaka 2025 na chaguo la kuongeza mwaka mmoja

Wakati huo huo, United bado wapo kwenye mazungumzo na kipa David De Gea kuhusu kuongeza mkataba wake.

Kipa huyo, ambaye alikuwa chauo namba moja kwa kocha, Erik ten Hag msimu uliopita, atakuwa mchezaji huru mara tu mkataba wake utakapokamilika Juni 30 lakini klabu hiyo inamtaka abaki.

United wanatumani kukubaliana kuongeza muda ambao utamsaidia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kupunguza kwa kiasi kikubwa mshahara wake wa kimsingi, lakini na bonasi za ndani kulingana na kiwango cha michezo anachocheza.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba hata kama De Gea atasalia, Ten Hag angependa kusajili kipa mwingine msimu huu wa joto ili kumpa Mhispania huyo ushindani zaidi kwa nafasi yake.

Jack Butland, ambaye aliwasili kwa mkopo kutoka Crystal Palace Januari, amesajiliwa na Rangers, lakini Tom Heaton atasalia United baada ya klabu hiyo kuamsha chaguo la mwaka mmoja katika mkataba wake.

# RONALDO ANAINUFAISHA URENO - MARTINEZ



**LISBON,** Ureno

KOCHA wa Ureno, Roberto Martinez anaamini kwamba Cristiano Ronaldo kucheza katika klabu isiyo ya Ulaya kutainufaisha timu ya taifa.

Huku kukiwa na taarifa kwamba anaweza kurejea kucheza Ligi ya England, mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or mara tano hivi karibuni alithibitisha kuwa atasalia Saudi Arabia na Al Nassr msimu ujao.

"Kucheza katika klabu isiyo ya Ulaya wakati mwingine ni faida unapocheza katika timu ya taifa," alisema Martinez.

Ronaldo alifunga mabao 14 katika mechi 16 tangu ajiunge na Al Nassr Januari baada ya kufutwa mkataba wake na Manchester United kwa makubaliano.

Mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi Ureno, Ronaldo mwenye umri wa miaka 38, amebakiza mechi mbili kufikisha mechi 200 akiwa na timu yake ya taifa.

"Tuna njia tatu za kuchambua mchezaji: ubora wa mtu binafsi, uzoefu na kujitolea," Martinez alisema.

"Ahadi ya Cristiano imekamilika. Yeye ni mfano kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, mfano kwa soka la Ureno na dunia. Ameichezea timu ya taifa mechi 198."

Nyota huyo wa zamani wa Real Madrid na Juventus anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi ya kimataifa, akiifungia Ureno mabao 122 tangu alipocheza kwa mara ya kwanza mwaka 2003.

"Cristiano na beki mkongwe wa FC Porto, Pepe ni mifano ya soka la Ureno, na tunawahitaji kupitisha uzoefu na hekima kwa wachezaji wachanga zaidi," aliongeza Martinez.


"Kama mchezaji mwingine yeyote, (Ronaldo) anahitaji kufanya mazoezi vizuri ili kucheza. Tunahitaji mazingira ya kiwango cha juu na ushindani kwa wachezaji wetu."

# *Walker aingia kwenye rada za Bayern Munich*

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich ipo kwenye mazungumzo na Kyle Walker kuhusu kuhamia Allianz Arena huku Manchester City wakiwa tayari kumtoa beki huyo wa pembeni aliyeshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, vyanzo vimeiambia ESPN.

Walker mwenye umri wa miaka 33 yuko chini ya mkataba Etihad hadi mwisho wa msimu ujao, lakini mazungumzo ya kuongeza mkataba kwa beki huyo wa England bado hayajaendelea.



Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Walker yuko tayari kuhamia Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, ili kupanua taaluma yake katika kiwango cha juu baada ya kuchanganyikiwa na kukosekana kwa ofa thabiti kutoka kwa City kujadili masharti mapya.

Beki huyo wa zamani wa kulia wa Sheffield United, ambaye pia anavutiwa na Saudi Arabia, alitolewa kwenye ushindi wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Inter Milan mjini Istanbul wiki iliyopita huku kocha, Pep Guardiola akiamua kumtumia Manuela Akanji kama beki wa pembeni.

Guardiola hapo awali alitilia shaka matarajio ya muda mrefu ya Walker katika klabu ya City kwa kusema kwamba mchezaji huyo, aliyesajiliwa kwa pauni milioni 45 kutoka Tottenham Hotspur mwaka 2017, hakuweza kuzoea mfumo mpya wa kimbinu ambao ulipelekea John Stones kupendekezwa kuanza mbele yake.

Lakini ingawa Walker alirudisha nafasi yake kwenye kikosi na alikuwa bora katika ushindi wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid, na haswa katika vita vyake vya moja kwa moja na winga Vinicius Junior, vyanzo vimesema kwamba Guardiola sasa yuko tayari kupanga maisha yajayo kwa kumtoa Walker.

City wanakabiliwa na msimu wa joto wa hali ya juu huku beki wa kimataifa wa Ureno João Cancelo pia akitarajiwa kuondoka baada ya kutumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo Bayern.

Pia kuna mashaka makubwa juu ya mustakabali wa nahodha Ilkay Gündoğan, ambaye mkataba wake unaisha mwishoni mwa mwezi huu.

HABARI MICHEZO

# TAIFA STARS INA KILA SABABU YA KUSHINDA LEO

Na Saada Akida

TIMU ya taifa 'Taifa Stars' ina kila sababu ya kushinda kwenye mchezo wa leo wa kufuzu fainali za AFCON dhidi ya Niger kwenye uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mchezo huo utapigwa leo kuanzia saa 10:00 alasiri, Stars wapo kundi F linaloongozwa na Algeria wakiwa na alama 12, Tanzania inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi 4 sawa na Uganda inayoshika nafasi ya tatu, Niger inashika nafasi ya mwisho.

Kuelekea mchezo huo kocha msaidizi wa Taifa Stars, Hemed Moroko alisema ni mchezo muhimu sana na wanahitaji kupata matokeo ili kuweka hai matumaini yao ya kufuzu fainali za mwakani za AFCON.

Alisema wamewafuatilia Niger katika michezo mbalimbali waliyowahi kucheza na kuona madhaifu na ubora wao na wamejipanga vizuri kwa ajili ya kusaka ushindi katika mchezo wa leo.

"Tumekuwa na madhaifu yetu katika mechi iliyopita na Uganda na kufanyia kazi, kwa sasa tuko vizuri hasa safu ya ushambuliaji hatukuwa na umakini mzuri na sasa tunaamini mechi ya leo tutatumia vizuri nafasi tutakazozitengeneza ," alisema Moroko na kuongeza.

"Niger sio timu mbaya kwa tulivyowaona, tunaenda kucheza mechi hiyo kwa nidhamu ya hali ya juu, kwa sababu tunaimani na wachezaji tuliowaita tunaweza kufanya vizuri kwa kupata ushindi na alama tatu zitakazotuweka katika nafasi nzuri kutengeneza matumaini ya kufuzu," alisema Moroco.

Aidha alisema wameongea na wachezaji wao na kuwajenga kisaikolojia ili kupata ushindi kwenye mchezo wa leo.

Kwa upande wake kiungo wa timu hiyo, Himid Mao alisema wako tayari kwa mchezo wa leo na watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kuweza kuipeperusha vyema Tanzania.

"Tunahitaji kufanya vizuri lakini kupata matokeo hayo lazim kupata sapoti kwa watanzania kwa kutuunga mkono kwa ajili ya kupata matokeo mazuri, mechi iliyopita dhidi ya Uganda imekuwa deni kwetu kwa watanzania kwa sababu ya kutofanya vizuri katika mchezo huo," alisema," alisema Himid.

Mechi ya mwisho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Taifa Stars ilikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Uganda




Wachezaji wa KMC wakishangilia moja ya goli walilofunga dhidi ya Mbeya City juzi kwenye mchezo wa mchujo kuwania kubaki Ligi Kuu msimu ujao, KMC walishinda mabao 2-0. **PICHA: BINZUBERY**

# *Simba SC yaanza makeke...*

INATOKA UK. 24

tous), Saido (Ntibazonkiza) basi mambo yataenda vizuri na Baleke atafunga sana, " alisema Kazungu.

Alisema licha ya Onana kutoka kwenye ligi ndogo ukilinganisha na Tanzania, bado atakuwa na msaada mkubwa kwenye kikosi cha Simba.

Mkuu wa Kitengo cha habari na Mawasiliano cha Simba, Ahmed Ally alisema mambo yote ya usajili uongozi utatoa taarifa yake rasmi kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

"Wanasimba wasubiri taarifa rasmi ya viongozi, lakini niwahakikishie Simba itafanya usajili bora kwa manufaa ya timu," alisema Ahmed.

Simba inatarajiwa kushiriki mashindano ya Super Cup ikiungana na timu nyingine saba zilizoteuliwa na CAF kushiriki michuano hiyo.

## Julio atamba KMC itatisha msimu ujao

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kufanikiwa kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuifunga Mbeya City mabao 2-0 kwenye mechi ya 'play off' juzi Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Kocha wa KMC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema anataka kuitengeneza timu hiyo iwe ya kutisha msimu ujao.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo kumalizika, Julio ambaye aliichukua KMC ikiwa kwenye hali mbaya kiasi cha kwenda kwenye mechi za mchujo, ameonyesha kufurahishwa kubaki Ligi Kuu, huku akiahidi kukisuka vyema kikosi chake kwa ajili ya kuleta upinzani msimu ujao.

"Mwakani sasa ndiyo mtamuona Julio, tutakuwa Ligi Kuu na timu itakuwa imeboreshwa kwa ajili ya kutoa ushindani," alisema.

Aidha aliwashukuru viongozi wa KMC kwa msaada na sapoti kubwa waliyompa hadi kufanikiwa kusalia Ligi Kuu.

"Nawashukuru viongozi wote wa KMC, wamepambana kwa kila hali, tulidhamiria KMC kubakia kwenye ligi, ila Mbeya City hawakuwa waungwana, tukiwa kwao walipiga wachezaji wetu, wametufanyia mambo mengi ya kihuni, lakini sisi hatukulipa kisasi, azma yetu ilikuwa kupata bao moja mapema ndani ya dakika 10, tukalipata kwenye dakika ya tatu tu, tukalilinda, baadaye tukapata la pili, bao hilo lilitupa presha sana kwa sababu tulijua wakifunga moja tu tunakwenda kwenye penalti, nikawa natamani wachezaji wangu wafunge la tatu, haikuwezekana na wao hawakupata bao," alisema Julio kwa furaha.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mbeya City, Abdallah Mubiru alisema kinachofanyika sasa ni siasa za mpira na si mpira wa uwanjani.

"Hakuna kipya, tulijua nini kinakwenda kutokea, nini waamuzi wanakwenda kufanya kwa sababu kimepangwa, tutaangalia nini tutafanya kwenye mechi inayokuja ya 'play off dhidi ya Mashujaa FC, sisi tutakwenda kucheza lakini bado kuna waamuzi pia, sisi tunajenga nje ya kiwanja wao ndiyo wanaamua nani atakwenda, sasa hivi siasa ndiyo zimeingia na si mpira tena," alilalamika Mubiru raia wa Uganda.

KMC ilipata mabao yake kupitia kwa Daruweshi Saliboko na Awesu Awesu waliyoifanya timu hiyo kubaki Ligi Kuu kwa jumla ya mabao 3-2, Jumanne iliyopita KMC ilifungwa mabao 2-1 ikiwa ugenini, Uwanja wa Sokoine Mbeya.

Kwa matokeo hayo, Mbeya City inakwenda kucheza 'play off' ya mwisho dhidi ya Mashujaa FC ya ligi daraja la kwanza 'Championship', ambapo kama ikishinda itabaki Ligi Kuu na ikifungwa itashuka daraja.

Hii ni mara ya pili kwa Mbeya City kwenda kucheza 'play off' na timu ya Championship, msimu wa 2019/20 ilicheza dhidi ya Geita Gold na kufanikiwa kubaki kwa jumla la mabao 2-1, ikitoa sare 1-1 ugenini na kushinda bao 1-0 nyumbani.

## Yanga: Tunahitaji kocha mwenye mataji Afrika

INATOKA UK. 24

alisema.

Alisema bado wapo kwenye mchakato wa kumpata kocha mkuu wa Yanga na mashabiki waendelee kuwa watulivu watatangaziwa kocha mpya.

Hata hivyo, taarifa zinasema Ibenge ndiye ambaye anapewa nafasi kubwa kumrithi Nabi, wengine wanaohusishwa ni Juan Carlos Garrrido kutoka Hispania, Watunisia Fouuzi Benzarti, Nabil Maaloul na Julien Chevalier kutoka Ufaransa.

# Michezo


Jumapili Juni 18, 2023

Nipashe




## Messi: Nasubiri kucheza Marekani

UK. 21




Mwenyekiti wa bodi ya klabu ya Simba Salim Abdallah 'Try Again' (wa mwisho kulia) kwenye picha ya pamoja na mdhamini mpya wa jezi wa klabu hiyo Yusuph Yenga (wa pili kushoto) wakishika mfano wa hundi ya udhamini kwa klabu hiyo juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Simba SC yaanza makeke yamsajili Mcameroon

●●● Ni nyota aliyekuwa akikipiga klabu ya Rayon Sports ya Rwanda, kunogesha kikosi msimu ujao...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeanza makeke ya usajili baada ya kukamilisha dili la kumchukua Winga wa kushoto wa Rayon Sports ya Rwanda raia wa Cameroon, Andre Onana Esombe ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo.

**Taarifa kutoka nchini Rwanda kutoka vyanzo mbalimbali vya habari vinasema tayari Simba imeshamalizana na mchezaji huyo kwa ajili ya msimu ujao wa ligi, huku akitajwa kuwa atakuja kuwa msaada mkubwa kwa klabu hiyo.**

Taarifa zinasema kuwa Simba imemsajili mchezaji huyo kwa uhamisho wa Sh. Milioni 417 na wakala wake ndiye aliyefanikisha dili hilo baada ya nyota huyo kutakiwa na klabu mbalimbali za Afrika na nje ya Afrika.

Akizungumza na gazeti hili, Mwandishi wa habari na mchambuizi wa soka nchini Rwanda, Claver Kazungu alisema Simba imelamba 'dume' kwa kumsajili nyota huyo.

"Ndiyo inasemekana thamani yake ni dola laki moja na nusu hivi au zaidi, kuna timu Uarabuni zilikuwa zinamuhitaji mpaka dola laki tatu na yeye alikuwa anahitaji kwenda kucheza kwenye pesa nyingi, wakala wake akamshauri ni vyema akacheze klabu ya Simba kwa sababu itacheza michuano ya Super League ili iweze kumsaidia hata kuitwa kwenye timu ya taifa ya Cameroon, kwa hiyo kwa umri wake wa miaka 23 ana muda mrefu wa kucheza soka," alisema Kazungu.

Alisema mchezaji huyo ana uwezo mkubwa na kama akifika na kufuata kilichompeleka anaweza akawa kipenzi cha mashabiki wa Simba.

"Ni fundi wa mpira, niamini mimi, labda ikitokea tu, maana kuna baadhi ya wachezaji wakifika Tanzania wanashindwa kucheza mpira kutokana na mazingira ya nje ya uwanja kama ataepuka mambo ya nje ya uwanja nina uhakika akiungana na akina Chama (Cla-

INAENDELEA UK. 23

## Yanga: Tunahitaji kocha mwenye mataji Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema upo makini katika mchakato wa kusaka kocha Mkuu na wameweka malengo ya kumpata kocha mwenye uwezo mkubwa na aliyefanikiwa kupata mataji Afrika.

Yanga ipo kwenye mchakato wa kusaka kocha mpya baada ya aliyekuwa kocha wao Nasreddine Nabi kugoma kuongeza mkataba mpya na anatajwa kujiunga na klabu ya Kaizer Chief ya Afrika Kusini.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Habari na klabu hiyo, Ali Kamwe amesema kitu cha kwanza wanachoangalia ni uwezo wa kocha na mataji ambayo amefanikiwa kuyapata akiwa na klabu nyingine.

"Sifa zipo nyingi za kocha anayetakiwa na Yanga, lakini namba moja ni mwenye mataji, nawaambia makocha wote ambao wametuma CV, kama hawana mataji kwenye klabu walizitoka, angalau moja tu, we soma Uefa, Class A, B, D mpaka F, Q hadi Z, kama huna mataji hapana, kwa sababu sisi ni timu ya kunyanyua makwapa karibuni kila msimu," alisema Kamwe.

Ofisa Habari huyo hakukanusha wala kukataa kwamba makocha wawili wakubwa Afrika, Mkongomani Florent Ibenge na Msauzi Afrika, Pitso Mosimane kutuma maombi yao kwenye klabu hiyo.

"Ukizungumza mmoja wa makocha wenye mataji ni Ibenge, alichukua Kombe la Shirikisho akiwa na RS Berkane ya Morocco, Mosimane, kafanya vizuri akiwa na Mamelodi Sundowns pale Afrika Kusini, kafanya vyema akiwa na Al Ahly kule Misri, ni mwenye mafanikio na mataji, kama watu wanaihusisha Yanga na makocha hao ni kwamba wameshajua kuwa tunahitaji makocha wenye mataji, baada ya Nabi kuondoka makocha wengi wametuma CV, hii inaonyesha kuwa Yanga ni timu ambayo kwa sasa inafuatiliwa sana Afrika,"

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >